




UKURASA 3

## TPA yashiriki mkutano Zambia kuhusu shehena


Viberenge milimani vitatutumbukia nyongo!

BUFE

IJUMAA FEBRUARI 25, 2022 Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

MJUE KIJANA LINDA

Aonyesha ishara ya kuigwa kujiajiri akibuni 'NGO' yenye mazito mtaani

Bodi ya Pamba inavyopambana katika safari ngumu kunasua wakulima wake


# Nipashe

Ijumaa Februari 25, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580867

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardi...


UKURASA 11

# 43% ya chumvi nchini ni hatari


Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Prof. Abel Makubi



**WIZARA** yaonya ongezeko la goita, watoto njiti... *Endelea ukurasa 2*

UKURASA WA 5

### BASHE ATANGAZA FURSA UWEKEZAJI KATIKA KILIMO

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe, amesema Tanzania iko tayari kushiriki-ana na kampuni...

UKURASA WA 5

### WANAFUNZI 4,060 HAWAJARIPOTI KIDATO CHA KWANZA

WANAFUNZI 4,060 waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2022 mkoani Rukwa, hawajaripoti ...

## Mwanafunzi aandika barua kuacha shule

UKURASA 3


Askofu Dk. Fredrick Shoo

## Askofu ashangaa walinzi wa raia kutuhumiwa mauaji

UKURASA 2


Form 281d

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
BUSINESS REGISTRATIONS AND LICENSING AGENCY

Advertisement of Winding-up Petition
Pursuant to Rule 99(1) of the Companies (insolvency) Rules 2005
Misc. Commercial Case No.42 of 2021

IN THE MATTER OF: BAHDELA CO. LIMITED

A Petition to wind up the above-named Company of:

Address: The Registered office of the Company is at Plot No.186053/23, Upanga Street, P. O. Box 5950, Dar es Salaam, Tanzania.

presented on: 31ST AUGUST, 2021

by: (name and address of petitioner) PETROFUEL (T) LIMITED OF P.O.BOX 14525, PLOT NO.33/1 & 34/1, MBAGALA INDUSTRIAL AREA, DAR ES SALAAM, TANZANIA

Claiming to be a [creditor] of the Company, is fixed for orders at (Name of Court) THE HIGH COURT OF TANZANIA, COMMERCIAL DIVISION AT DAR ES SALAAM

on (date): 10TH MARCH 2022

at (time): 9:00AM IN THE MORNING
(or as soon thereafter as the petition can be heard)

Any person intending to appear on the hearing of the Petition (whether to support it or to oppose it) must give notice of his intention to do so to the petitioner or his/its Advocate in accordance with Rule 104(1) of the Companies (Insolvency) Rules 2005 by 16:00 hours on the business day before the date of the hearing given above.

The Petitioner's Advocate is: S. Ishengoma, SA Law Chambers, Advocates, PPF Tower, 4th Floor, Ohio /Garden Avenue Street, P.O. Box 22691, Dar es Salaam
Mobile: 0786222242
Email: adv.ishengoma@gmail.com, s.ishengoma@salawchambers.co.tz
(REF: SI/108/PFL)

Dated 8th February, 2022.

216697102


**MICHEZO** YANGA YAFUNGUKA ILIPOISHIKA MTIBWA UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# 43% ya chumvi nchini ni hatari

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema asilimia 43 ya chumvi inayozalishwa nchini haichanganywi na madini joto na hivyo kuhatarisha afya za walaji ikiwamo kupata ugonjwa wa goita na kujifungua watoto njiti.

Kutokana na hali hiyo, serikali imekuja na mpango jumuishi ambao wazalishaji chumvi wanapaswa kujiunga kwenye vikundi ili kupatiwa mashine za kuchanganya madini hayo.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Prof. Abel Makubi, alibainisha hayo jana jijini hapo alipokabidhi mashine tano za kuchanganya madini joto kwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa ajili ya halmashauri zinazozalisha chumvi.

Alisema Tanzania ina uwezo mkubwa wa kuzalisha chumvi ambapo tani zaidi ya 300,000 zinazalishwa nchini kwenye maeneo mbalimbali lakini asilimia 43 haiwekwi madini hayo.

Prof. Makubi alisema serikali kwa kushirikiana na wadau, imetengeneza mashine ambazo kwa sasa zinapatikama VETA kwa gharama nafuu ili kusaidia wazalishaji kuchanganya chumvi na madini hayo.

"Wananchi wasitumie chumvi bila kuchanganywa na madini joto, kunasababisha madhara mengi ikiwamo goita na hata kujifungua watoto njiti," alionya.

Prof. Makubi alizitaka halmashauri zinazozalisha chumvi kusimamia kikamilifu wazalishaji kuchanganya chumvi na madini joto ili kuepukana na madhara hayo.

Katibu Mkuu Ofisi ya Rais TAMISEMI, Prof. Riziki Shemdoe, aliwataka makatibu tawala wa mikoa iliyopatiwa mashine hizo kuhakikisha zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa na sio kuzifungia.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Caroline Nombo, alisema kutokana na maboresho ya mafunzo na ufundi stadi nchini, VETA imetengeneza mashine hizo na kuokoa fedha za serikali ambazo zingetumika kuzinunua nje ya nchi.

Alisema uwapo wa mashine hizo utasaidia utekelezaji wa mwongozo wa lishe shuleni uliozinduliwa mwishoni mwa mwaka jana.

Awali Mkurugenzi wa Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC), Dk. Germana Leyna, alisema lengo la kutoa mashine hizo ni kuhakikisha asilimia 90 ya kaya zitumie chumvi yenye madini hayo.

"Taasisi yetu inatoa elimu na namna ya kuchanganya madini hayo na kupima. Kwa mwaka 2016/17, utafiti wa hali ya lishe unaonyesha asilimia 60 ya kaya zinatumia chumvi yenye madini joto na utafiti wa mwaka 2018 ulionyesha bado hatujapiga hatua," alisema.

Alibainisha kuwa mwaka 2019 utafiti ulifanyika wa kiwango cha uzalishaji chumvi na uwekaji wa madini joto ambapo ilionyesha Tanzania inazalisha tani zaidi ya 337,000 kwa mwaka na asilimia 57 tu ndiyo yenye madini.

"Taasisi kwa kushirikiana na wadau ilianzisha mchakato wa kuwajengea uwezo wajasiriamali wadogo ambao utafiti unaonyesha ndiyo wanaochangia kwa kiwango kikubwa kuzalisha chumvi ambayo haina madini joto," alisema.

Aliongeza kuwa mwaka 2019 zilinunuliwa mashine tatu kutoka Afrika Kusini kwa gharama ya Sh. milioni 25 kila moja na kuzisambaza.

"Kwa sasa kwa kushirikiana na VETA, tumetengeneza mashine tano ambazo gharama yake ni nusu ya gharama iliyotumika kununua mashine moja Afrika Kusini," alisema.

Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Nutrition International, Dk. Daniel Nyagawa, ambao wametoa mashine hizo, alisema zitasimikwa katika mikoa ya Tanga, Pwani na Mtwara.

Alisema katika mpango mkakati wake wa miaka sita ulioanza mwaka 2018 hadi 2024, shirika hilo limejielekeza kufanya kazi zake kwa karibu na serikali na taasisi zake ili kwa pamoja kupambana na utapiamlo na madhara yatokanayo na utapiamlo.



Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko (kulia), akizungumza na wananchi wa kijiji cha Maskati, wilayani humo juzi, ambao mashamba yalipitiwa na mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR), kipande cha tano kutoka Mwanza hadi Isaka, Wilayani Kahama na kuwahakikishia kuwa wote watalipwa fidia. **PICHA: MARCO MADUHU**

## Watuhumiwa wa ugaidi waachiwa kwa dhamana

**Na Abdallah Khamis,** MTWARA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Mtwara, imewaachia kwa dhamana washtakiwa watatu waliokuwa wanakabiliwa na mashtaka ya ugaidi tangu mwaka 2017.

Walioachiwa huru ni Moshi Kakoso, Waziri Selemani Mkaliaganda na Omari Bumbo, ambao kesi yao ilikuwa inasikilizwa na Hakimu Musa Esaju.

Hakimu Mkazi Esaju alisema washitakiwa hao wameachiwa baada ya kutimiza vigezo vya dhamana hiyo ambayo ni kila mmoja kuwa na wadhamini wawili wenye kuweka ahadi ya Sh. milioni 20 kwa kila mdhamini.

Aidha, wametakiwa kuripoti katika Ofisi ya Mkuu wa Upelelezi Mkoa wa Mtwara, kila wiki ya mwisho kwa kila mwezi kwa muda wa miaka mitatu. Masharti mengine ni kutunza amani katika kipindi chote watakachokuwa chini ya udhamini.

Hakimu Esaju alisema baada ya Jamhuri kujiridhisha kuwa wametimiza vigezo vya kupewa dhamana washtakiwa hao wameachiwa.

Alisema washtakiwa hao watakuwa chini ya uchunguzi na uangalizi wa vyombo vya ulinzi na usalama wakifuatiliwa nyendo zao kwa muda wote wa dhamana yao.

Aliongeza kuwa hawatatakiwa kutenda vitendo vya jinai, lengo likiwa ni kutunza amani na iwapo watavunja makubaliano hayo watarudishwa mahakamani na kuendelea na kesi yao iliyofutwa.

Mbele ya Hakimu huyo, Wakili wa Serikali Mkuu, Mwahija Ahmed, alidai kuwa Jamhuri haina nia ya kuwashtaki washitakiwa hao katika kesi yao ya ugaidi.

Awali, ilidaiwa mahakamani hapo kuwa watatu hao walikula njama na kutenda ugaidi kwa kujiunga na kikundi kisichosajiliwa cha Hisbu Tahir ambacho shughuli yake ni kushawishi watu kujiunga na kutaka kuanzisha dola ya kiislam ndani ya Tanzania.

Washtakiwa hao walikamatwa mwaka 2017 katika maeneo tofauti tofauti ya mikoa ya Dar es Salaam na kufunguliwa kesi hiyo namba 09/2017 iliyokuwa ikisubiri upelelezi ukamilike ili ihamishiwe Mahakama kuu (PI).

# Askofu ashangaa walinzi raia kutuhumiwa mauaji

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MKUU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Fredrick Shoo, amesema inasikitisha wenye jukumu la kulinda raia na mali zao wanatajwa kwenye matukio ya mauaji.

Alitoa kauli hiyo jana mjini Moshi wakati wa kikao cha Kamati za Interfaith kilichofanyika mkoani Kilimanjaro na kuwajumuisha viongozi wa dini wa Kanda ya Kaskazini.

"Kama mnavyosikia katika jamii yetu kwa sasa kuna mauaji ya ajabu ajabu yamezuka, mara unasikia watoto wanaua wazazi, mama anaua watoto, mume anaua mke na mke anaua mume, mara watu wanajinyonga na hali ya kusikitisha zaidi hata wale tuliowaamini kuwa wanaweza kutulinda wamegeuka kuwa wauaji na watesaji wetu na wanatajwa katika mauaji," alisema Askofu Dk. Shoo.

Alisema ni wajibu wa viongozi wa dini kumwomba Mungu aondoe roho ya mtu kuona kuondoa uhai wa mtu ni jambo la kawaida, kwamba anaweza kuuondoa anavyotaka yeye.

"Katika hali kama hii sisi viongozi wa dini tushikamane katika kuiombea jamii yetu, tunahitaji sana kuomba na kukemea matendo maovu, pia tuwe mstari wa mbele katika kuhakikisha tunakemea roho ya wanajamii kutojali hali ya kutoa roho za wenzao," alisema.

Askofu Shoo alisema ni wakati umefika jamii ielimishwe namna ya kuthamini na kutunza uhai, huku wakiendeleza kupaza sauti ili kukemea vitendo vya kikatili vinavyoendelea katika jamii.

"Tunaiomba serikali yetu kushughulikia ipasavyo wale wote wanaobainika kushughulika na matendo maovu katika jamii, hasa suala la mauaji.

"Pia serikali isimamie maadili ya watumishi wake na hasa hawa wa vyombo vya usalama ili waweze kulinda uhai wa wananchi na mali zao, na inapotokea vyombo vya usalama vikahusika na matendo maovu na hasa mauaji kama yalivyotokea huko Mtwara, wananchi wanakosa kabisa matumaini na serikali yao," alionya.

Kiongozi huyo wa kiroho alisema hali hiyo inawafanya wananchi wakose sehemu ya kukimbilia na badala yake, kujichukulia hatua za kisheria.

"Serikali na watu wote tuitetee haki na kuhakikisha haki inatendeka, maana ni kwa njia hiyo amani yetu itastawi. Sisi viongozi wa dini tuna wajibu mkubwa wa kutetea haki na amani katika nchi yetu, tuendelee kuhimiza maadili mema, siyo tu kwa viongozi bali kwa raia pia," alisema.

Askofu Shoo alisema inasikitisha kuona kuwa vitu vya ajabu vinatokea na kuhusisha viongozi wenye dhamana na wanaoheshimika katika jamii ambavyo viongozi wa dini hawawezi kuvitamka.

"Serikali inapaswa kuwaondoa viongozi hao madarakani ili kulinda imani ya jamii yetu, viongozi tusichoke kuhimiza haki, amani, maadili na mshikamano bila kujali tofauti za dini zetu, ili kwa njia hii sauti yetu ya kupinga maovu iwe kubwa zaidi, tumejifunza katika umoja huu yapo mambo ambayo tunapaswa kusema bila woga, tumewekwa kama wasimamizi wa mambo haya," alisema.

Dk. Shoo aliwataka viongozi wa dini kuendelea kuomba kwa kuwa kuna alichokiita 'pepo la mauaji' linaloendelea kuleta laana kwenye ardhi pamoja na kuwahamasisha wananchi kutumia mvua inayonyesha kuotesha miti ili kutunza mazingira.

Askofu wa KKKT Dayosisi ya Kanda ya Kaskazini Magharibi Tanga, Dk. Msafiri Mbilu, alisema imefika wakati jamii kuacha kujichukulia sheria mkononi na serikali kusimamia haki.

"Viongozi wa dini tutasema na kuendelea kuhimiza maadili katika jamii, ila tunaomba serikali iache kufumbia macho matendo maovu yanayofanya ya watumishi walioko chini yake, kwani wananchi wanapochoka hujichukulia sheria mkononi," alitahadharisha.

Akitoa salamu za Mkoa wa Kilimanjaro, Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Kilimanjaro, Stephen Kagaigai, aliwataka viongozi wa dini kuhakikisha wanaendelea kuielimisha jamii juu ya kuporomoko wa maadili ili kulinda amani ya taifa.

"Maadili yameanza kuporomoka kuanzia ngazi ya familia, hivyo viongozi wa dini tuendelee kupaza sauti kwenye mimbari zetu ili jamii irudishe utamaduni wetu, kwa kufanya hivyo tutaepukana na matendo maovu yanayoendelea kulikabili taifa letu," alisema.



Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, Selemani Kakoso, akizungumza wakati wa ziara ya kamati hiyo, katika Bandari ya Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# TPA yashiriki mkutano Zambia kuhusu shehena

**Na Mwandishi Wetu**

UJUMBE wa Mamlaka ya Bandari (TPA) ukiongozwa na Balozi wa Tanzania Zambia, Hassan Yahaya, uko Zambia kushiriki katika moja ya mikutano muhimu ya wadau wa usafirishaji wa kimataifa wa shehena za Zambia.

Lengo la kushiriki katika mkutano huo ni kushawishi ongezeko la matumizi ya Bandari ya Dar es Salaam na wasafirishaji shehena za Zambia.

Ujumbe huo wa maofisa wakuu wa masoko na uhusiano umepania kutumia fursa za mkutano huo kutangaza ufanisi wa bandari za TPA baada ya uwekezaji mkubwa unaoendelea kufanywa na serikali katika miundombinu na vitendea kazi.

Katika mkutano huo, TPA inakutana na kampuni kubwa zinazojihusisha na usafirishaji wa mizigo ya Zambia kama Freight Africa, Afcons Infrastructure Ltd, Bridge Shipping (Z) Ltd, Longlihua Company Limited, Highrock Foundation, Siibwata Trading Investment Ltd, wizara na taasisi mbalimbali ikiwamo wizara za serikali ya nchi hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa zilizopatikana kutoka Lusaka jana, Balozi Yahaya ambaye amejiunga na ujumbe huo akimwakilisha Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Gabriel Migire, alisema kuna mabadiliko makubwa ya kiutendaji katika bandari za Tanzania baada ya uwekezaji uliofanywa na serikali. Akizungumza katika mkutano huo uliofunguliwa na Waziri wa Usafirishaji na Lojistiki wa Zambia, Frank Tayali, Balozi Yahaya alisema uwekezaji uliofanywa, umeleta mabadiliko ya kiutendaji na kuongeza ufanisi na uwezo wa kupokea, kupakua na kusafirisha bidhaa.

Yahaya akizungumza kwa niaba ya Serikali ya Tanzania, alisema bandari zake kubwa za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara sasa zina uwezo mkubwa katika kushughulikia shehena za aina zote kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa na serikali ambao unahitaji kutangazwa na kufanyiwa kampeni kubwa za kimasoko ili kupata shehena zaidi. Uchumi wa Zambia unaotegemea sana uzalishaji wa shaba, huisafirisha kwenda Uswizi, China, Singapore na unaagiza bidhaa nyingi za salfa, mafuta na bidhaa nyingine kutoka Afrika Kusini, China, Umoja wa Falme za Kiarabu. Emirates na Kuwait.

Hata hivyo, imeelezwa mkutanoni huko kwamba katika kipindi cha miaka mitano (2016/17 hadi 2020/21) shehena za Zambia zimekuwa zikipungua kwa wastani wa asilimia 10 kwa mwaka, ambapo uagizaji ulipungua kwa wastani wa 13 kwa mwaka, huku mauzo ya nje yakiongezeka kwa wastani wa asilimia 15 kwa mwaka.

Ujumbe wa Tanzania utakuwa na kazi kubwa ya kueleza mafanikio ya bandari za Tanzania baada ya ukarabati mkubwa na maboresho katika vitendea kazi na usalama wa bandari za Tanzania ambazo sasa ulinzi unafanyika kwa kutumia TEHAMA.

Zambia katika mkutano huo wameelezwa kuwa kuna faida kubwa ya kutumia Bandari ya Dar es Salaam dhidi ya bandari shindani kwa kuwa na njia ya reli ya moja kwa moja kutoka Bandari ya Dar es Salaam hadi ukanda wa shaba Zambia kwa ni njia muhimu ya utoaji na uingizaji wa bidhaa mbalimbali wa kutoka duniani kote ikiwa ni pamoja na mafuta, vifaa, makaa ya mawe, mbao, mbolea na pembejeo nyingine muhimu.

Mtandao huo una uwezo wa kuhudumia zaidi ya tani milioni 1.6 kwa mwaka.

Soko la Zambia linatafutwa kwa sababu ni rahisi kusafirisha shehena ya shaba ambayo inachangia asilimia 70 ya uzalishaji wa Afrika na zaidi ya asilimia 60 ya jumla ya mauzo ya nje ya nchi.

Meneja Masoko wa TPA, Lydia Mallya, alisema Bandari ya Dar es Salaam ndiyo lango kuu la mizigo si tu kwa Tanzania Bara na Ukanda wa Maziwa Makuu, bali pia kwa majirani wa Afrika Mashariki na Kati kama Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Malawi, Rwanda, Uganda na Zambia, na kwa mwaka 2021 ilisafirisha tani milioni 17.8.

Aliwaambia wajumbe wa mkutano huo kwamba kwa uwezo wa kuhudumia magari 600,000 kila mwaka, gati mpya ya urefu wa mita 320 katika Bandari ya Dar es Salaam hivi karibuni ilivunja rekodi yake ya kuhudumia na ya bandari nyingine zote za Mashariki na Kusini mwa Afrika kwa kukaribisha meli ya mizigo ya MOL Tranquil Ace yenye magari 3,743.

"Kutokana na kuongezeka kwa biashara ya baharini na kuongezeka kwa mahitaji ya soko, TPA imejipanga kukabiliana na hali hii inayokua kwa kasi kwa kutengeneza uwezo wa kukabiliana na mahitaji," alisema Lydia.

Alibainisha kuwa moja ya miradi hiyo ni wa Lango la Bahari la Dar es Salaam (DMGP) wenye thamani ya Sh. bilioni 336.4 na unawakilisha uboreshaji wa bandari ya kwanza kwa kiwango kikubwa katika historia yake.

Alisema mradi huo unaendelea vizuri, ambapo kazi za awali zimekamilika chini ya usimamizi na usimamizi wa TPA ambayo baada ya kukamilika kwa Bandari ya Dar itakuwa na uwezo wa kuhudumia tani milioni 28 kwa mwaka.

Katika miaka 60 ya Uhuru, kumekuwa na ongezeko la shehena kupitia bandari zinazosimamia na TPA kutoka tani 1,185,000 mwaka 1961 hadi kufikia tani 117,716,429 mwaka 2020/21.

# Mwanafunzi aandika barua kuacha shule

**Na Abdallah Khamis,** MTWARA

MWANAFUNZI wa kidato cha kwanza Shule ya Sekondari Msimbati, mkoani Mtwara (jina linahifadhiwa), amemwandikia barua ya kuacha shule Mkuu wa Shule hiyo, Hamisi Sadala. Katika barua hiyo aliyoiwasilisha kwa mkuu wa shule akiwa amesindikizwa na baba yake mzazi, Salum Hamis, aliandika kuwa uamuzi huo ni wa wake na hakulazimishwa na yeyote.

Tukio hilo la mwanafunzi kukabidhi barua ya kukataa kusoma lilisimuliwa jana na Sadala wakati akichangia mada kwenye kikao kilichoitishwa na Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, na wadau wa elimu kufuatilia utekelezaji wa mpango kazi wa elimu. "Leo (jana) asubuhi wakati ninajiandaa kuja kwenye kikao hiki, kuna mwanafunzi alifika ofisini kwangu akiwa ameambatana na mzazi wake akanikabidhi barua hii kuwa hataki shule na kwamba uamuzi huo hakulazimishwa na mtu yeyote," alisema Sadala.

Alisema sababu ya mwanafunzi huyo kuandika barua ya kuacha shule imechangiwa na kaka zake wawili walioacha masomo wakiwa kidato cha pili na kujielekeza katika uvuvi wa samaki pasipo hatua za kisheria kuchukuliwa dhidi yao na wazazi wao.

Mwandishi wa gazeti hili, aliona sehemu ya barua hiyo iliyoonyeshwa katika mkutano huo wa wadau wa elimu ikiwa imeandikwa kwa mkono:

"Barua kwa Mwalimu Mkuu mimi... shule imenishinda, mimi basi kusoma sitaki kusoma. Nimeamua kutokana na hali yangu mwenyewe, hajanishauri mtu yeyote nimeamua mimi mwenyewe."

Kisha barua hiyo ikaendelea kwa herufi kubwa: "Niliyekupa ndiye mwenye barua, mimi shule basi siyo utani ni kweli naondoka sina nia mbaya."

Wadau wengine waliotoa maoni katika kikao hicho walieleza changamoto iliyopo na inayosababisha watoto kuacha shule kuwa ni ukosefu wa chakula cha mchana pamoja na umbali wa shule katika baadhi ya maeneo.

Pia walieleza baadhi ya wazazi wanawashawishi watoto wao waende shule kwa ajili ya kuandikwa jina na kuepusha mzazi asichukuliwe hatua za kisheria huku wakiwasisitiza kuacha shule pale wanapoona hali imetulia.

Akizungumzia tukio hilo, Jenerali Gaguti alisema moja ya malengo ya kielimu kwa mkoa huo ni kuondoa tatizo la wanafunzi kuacha masomo katika ngazi tofauti tofauti ya kielimu. Aliwaeleza wadau waliohudhuria kikao hicho kuwa Mkoa wa Mtwara uko nyuma ya ufaulu wa kitaifa na matokeo ya kitaifa yanaposhuka mkoa unakuwa umechangia.

"Tuna malengo saba kimkoa na mikakati iliyowekwa ni lazima itoe majibu ya muda mfupi na mrefu kuhakikisha tunafuta namba ya wasiojua kusoma na kuandika. Lakini pia tunamaliza hii hali ya wanafunzi kuacha masomo kabla ya kuhitimu elimu ya msingi inayoishia kidato cha nne," alisema Gaguti. Alisema katika kufanikisha hilo, kila baada ya miezi mitatu watafanya tathmini ya wapi walipofikia kwenye mikakati ya kukuza elimu kwa kupima kila eneo jinsi walivyotimiza wajibu huo. Jenerali Gaguti aliongeza kuwa mkoa huo utabeba gharama za mitihani yote ya majaribio ya madarasa yanayofanya mitihani ya kitaifa ya mchujo kwa ngazi tofauti kuanzia msingi hadi sekondari.

Naye Ofisa Elimu Mkoa wa Mtwara, Kiduma Mageni, alitaja baadhi ya malengo kati ya saba yaliyowekwa na mkoa huo kwenye elimu ni pamoja na kuhakikisha wanafunzi wanaofika darasa la tatu wanamudu kusoma kuandika na kuhesabu na lengo la pili likiwa ni kukabiliana na utoro shuleni.


MASETO AUCTIONEER & DEBT COLLECTOR LTD

## NOTISI/TANGAZO LA MNADA

Kwa idhini tuliyopewa na **FNB Bank Tanzania Limited, MASETO AUCTIONEER & DEBT COLLECTOR LTD** tunamtangazia mdaiwa au mteja wa benki tajwa hapo juu kulipa mkopo wake ndani ya siku 7 tangu kutolewa kwa tangazo hili kwenye gazeti. Kushindwa kufanya hivyo kutapelekea sisi kuuza dhamana ya mdaiwa aliyoiweka benki wakati anachukua mkopo kwa njia ya mnada wa binafsi (Private Sale). Mnada utafanyika mahali nyumba/dhamana iliko kama inavyoonesha hapa chini kwenye jedwali.

| S/N | JINA LA MTEJA/MDAIWA | AINA YA DHAMANA | DHAMANA MAHALI ILIKO | TAREHE YA MNADA NA MUDA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | FLORIAN ALEX TESHA | FIRST CHARGE LEGAL MORTGAGE RESIDENTIAL PROPERTY TITLE NO. 12642, PLOT NO. 406, BLOCK J, NJIRO AREA, IN ARUSHA | NJIRO | 04/03/2022 SAA: 05:00 ASUBUHI |

**Masharti ya mnada**

1. Mnunuzi atatakiwa kulipa 25% ya bei ya mnada mara baada ya nyundo ya dalali kutua.
2. 75% inayobaki itatakiwa kulipwa ndani ya siku 14.
3. Gharama za kuhamisha umiliki wa dhamana ni za mnunuzi
4. Dhamana itauzwa kama ilivyo

MAWASILIANO +255 765 999 000 AU +255 787 288 442




Wafanyakazi wa Barrick wakifurahia tuzo mbalimbali zilizotunukiwa kwa kampuni yao, wakati wa hafla ya usiku wa madini iliyofanyika jijini Dar es Salaam juzi. Barrick imetangazwa kuwa ndio inayoongoza kwa ulipaji wa kodi katika sekta ya madini nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yatoa angalizo kujipanga mvua kubwa

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imetoa tahadhari kwa wananchi, kamati za usimamizi wa maafa mikoa na wilaya na sekta mbalimbali kutokana na mvua ya msimu wa masika za mwezi Machi hadi Mei mwaka huu ambayo inatarajia kunyesha juu ya wastani, kuwa inaweza kuleta madhara.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Dk. Pindi Chana, alisema ofisi yake inaendelea kuratibu shughuli za maafa kwa kuhakikisha ushiriki wa wizara, idara, taasisi na mamlaka za mikoa na wilaya na asasi katika kuzuia na kupunguza madhara ya majanga na kuendelea kukabiliana na kurejesha hali pindi yanapotokea.

Waziri huyo alisema taarifa ya utabiri wa mwelekeo wa msimu wa mvua ya masika inaonyesha itakuwa juu ya wastani katika maeneo mengi, hivyo imeonekana kuna haja serikali na wadau kuchukua hatua stahiki kuhakikisha kunakuwa na matumizi bora pamoja na hatua za kupunguza madhara na kujiandaa kukabiliana na maafa endapo yatatokea.

"Utabiri uliotolewa ni mahususi kwa maeneo ambayo kupata misimu miwili ya mvua kwa mwaka ambayo ni Nyanda za Juu Kaskazini - Mashariki (Arusha, Manyara, Kilimanjaro), ukanda wa Pwani ya Kaskazini (Pwani, Dar es Salaam na Tanga), Kaskazini mwa Mkoa wa Morogoro, visiwa vya Mafia na Unguja na Pemba, Ukanda wa Ziwa Viktoria (Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga, Simiyu na Mara) pamoja na Kaskazini mwa Mkoa wa Kigoma," alisema.

Alibainisha kuwa mvua hiyo inatarajiwa kuanza mapema kati ya wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Februari na kuishia Mei.

Alisema utabiri uliotolewa unaonyesha kutakuwa na ongezeko la mvua katika kipindi cha Machi kwenye maeneo ya Pwani Kaskazini na Aprili kwa maeneo ya Nyanda za Juu Kaskazini-Mashariki.

"Hali hii inaweza kusababisha madhara katika sekta mbalimbali yakiwamo matukio ya magonjwa mlipuko kwa binadamu, wanyama, wadudu waharibifu wa mazao na mimea yanaweza kujitokeza kutokana na hali ya unyevu unyevu," alisema.

Dk. Chana alisema ongezeko la maji katika mabonde linaweza kusababisha maporomoko ya ardhi na kuathiri shughuli mbalimbali hususan maeneo ya wachimbaji wa madini wadogo.

Alisema vipindi vya mvua kubwa vinaweza kuambatana na mafuriko na kusababisha uharibifu wa miundombinu, madhara ya kiafya na upotevu wa mali.

Alisema Ofisi ya Waziri Mkuu imetoa maelekezo kwa kamati za usimamizi maafa za mikoa, wilaya, kata na vijiji au mitaa katika mikoa husika kuchukua hatua stahiki zenye lengo la kuzuia na kupunguza madhara yanayoweza kujitokeza na kujiandaa kukabili maafa.

"Ninaziagiza kamati za usimamizi wa maafa ziwajibike kutekeleza, kusimamia na kuchukua hatua, kuhakikisha mvua hizi zinatumika kwa shughuli za maendeleo zikiwamo kilimo, kuandaa mabwawa na malambo kwa ajili ya kuvuna maji kupanda mazao yanayohitaji maji mengi," aliagiza.

Pia aziagiza ziandae mipango ya kuzuia milipuko ya magonjwa kwa binadamu na wanyama na kwa upande wa idara na taasisi zinazohusika na miundombinu zihakikishe barabara zinapitika wakati wote, madaraja na mitaro nayo isafishwe.

Waziri huyo aliagiza sekta za maji na umeme ziweke mipango ya kuhakikisha madhara yanapewa ufumbuzi mapema.

Dk. Chana aliwataka wananchi wahamasishwe kuishi katika makazi na kutekeleza shughuli za uzalishaji katika maeneo salama.

Aliwataka wananchi wanaoendesha shughuli zao za kiuchumi pembezoni mwa mito na mabonde, wachukue tahadhari Ili kunusuru maisha yao na mali zao.

"Ikumbukwe kuwa madhara yanaweza kuongezeka endapo hatua stahiki hazitachukuliwa na kuzingatia ushauri wa kitaalamu. Serikali itaendelea kutoa taarifa kadri mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) itakavyotabiri," alisema.

Mkutano huo pia ulihudhuriwa na Mkurugenzi Mkuu wa TMA, Dk. Agnes Kijazi.

# Serikali kuzibana taasisi zake bajeti ya 2022/23

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imezindua timu ya kitaifa ya kuwezesha ugharamiaji wa miradi ya maendeleo kwa kutumia njia mbadala (APF) ambapo kuanzia mwaka ujao wa fedha (2022/23), taasisi za umma zikiwamo halmashauri zenye miradi inayokidhi vigezo vya njia hiyo, hazitapelekwa kwenye bajeti ya serikali kama ilivyozoeleka.

Utaratibu huo ni utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Maendeleo wa Sekta ya Fedha wa Mwaka 2020/21 hadi 202/30 ambao umeandaliwa na serikali kwa kushirikiana na wadau wa benki na taasisi za fedha katika kuhakikisha upatikanaji wa fedha za muda mrefu kwa ajili ya kugharamia miradi ya kimkakati.

Akizindua timu hiyo jana yenye wajumbe 31, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Lawrence Mafuru, alisema katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitatu, serikali imepanga kupata Sh. trilioni 40.6 kutoka sekta binafsi na jukumu la kufanikisha hilo lipo kwa timu hiyo.

Mafuru alisema ugharamiaji miradi hiyo kwa kutegemea bajeti ya serikali umekuwa na vikwazo mbalimbali ikiwamo ufinyu wa bajeti na kusababisha kutokamilika kwa wakati, hivyo kwa utaratibu huo ni mwarobani wa vikwazo hivyo.

"Naomba niseme tumeanza sasa mchakato wiki mbili zilizopita wa maandalizi ya bajeti ya serikali (2022/23), tutapokea miradi mingi kutoka kwenye taasisi mbalimbali zinazotekeleza miradi, ujumbe uwafikie kwenye miradi ile ambayo ina vigezo kwenda kwenye APF, tunaomba mtuonyeshe kwamba tumeenda huko tumeshindwa ndio turudi huku, lakini kama tunaweza tuna 'cash flow' au kutumia Diaspora Bonds, Infrastructure Bonds, tunashauri njia hizo zitumike," alisema.

Aliongeza kuwa mahitaji ya ugharamiaji miradi ya serikali yamekuwa makubwa huku mapato yanayotokana na vyanzo vyake yakikua taratibu kuliko ambavyo mahitaji yanaongezeka.

"Katika Mpango wa Maendeleo wa Pili ulioisha, ulitarajiwa kutekelezwa kwa Sh. trilioni 107 lakini malengo yake mengi hayakutekelezwa kama ilivyokuwa imepangwa na sababu kuwa ni vyanzo vya fedha.

"Hatuna control (udhibiti) ya vyanzo vya fedha, tunategemea sana hisani za wafadhili na kwa kuwa wanafanya kazi kwa sera zao, hakuna guarantee (uhakika) kwamba miradi ingekamilika kwa wakati," alisema.

Mafuru alisema serikali imejifunza kupitia hilo na kuamua kuja na ugharamiaji wa miradi kwa njia mbadala ambapo kwenye Mpango wa Maendeleo wa Tatu ambao unakadiriwa kugharimu Sh. trilioni 114.9. Kati yake, Sh. trilioni 40.6 zitatoka sekta binafsi.

"Tutaweka mazingira wezeshi ili sekta binafsi ishiriki kikamilifu bila shaka katika utekelezaji wa miradi hiyo, hivyo ni wazi kwamba utaratibu huu ni muhimu sana katika kipindi hiki ambacho serikali ina miradi hii ya kimkakati lakini pia ikiwa inaelekea kukamilisha ile awamu ya mwisho ya miaka mitano ya Dira ya Taifa ya Mwaka 2025," alisema.

Alisema timu hiyo itakuwa na jukumu la kujenga uwezo wa wizara, idara, taasisi, wakala, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kuandaa maandiko ya miradi na kufanya upembuzi yakinifu na kuratibu uandaaji wa maandiko ya miradi yatakayogharamiwa kwa njia mbadala na kuratibu utoaji wa elimu kwa umma.

Kaimu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Switbert Mkama, alisema kumekuwapo na miradi mingi nchini lakini ina kikwazo cha maandiko, hivyo kupitia timu hiyo anaamini itaibua miradi inayoweza kukopesheka.

Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Mitaji (UNCDF), Peter Malika, alisema shirika limetoa Sh. milioni 460 kama mtaji ili kuwezesha timu hiyo kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Mitaji na Dhamana wa Soko la Hisa Dar es Salaam (DSE), Nicodemus Mkama, alisema hadi sasa thamani ya uwekezaji kwenye soko hilo ni Sh. trilioni 32.

# Wanafunzi 4,060 hawajaripoti kidato cha kwanza

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

WANAFUNZI 4,060 waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2022 mkoani Rukwa, hawajaripoti shule kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo utoro.

Akizungumza jana kwenye mkutano wa wadau wa elimu, Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Joseph Mkirikiti, alisema waliripoti hadi sasa ni asilimia 80.2.

Mkirikiti alisema wanafunzi walioko shuleni hadi sasa ni 16,264 kati ya wanafunzi 20,324 waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza kwenye shule mbalimbali za sekondari mkoani Rukwa.

Mkuu huyo wa Mkoa aliwaagiza wadau wa elimu kuchunguza na kubaini sababu mbalimbali zinazowafanya wanafunzi hao kutojiunga shule na kutafuta mbinu za kumaliza changamoto hizo.

Pia aliwataka wazazi mkoani hapa kubadilika na kuona umuhimu wa elimu kwa watoto wao kwa kuwa wao wanahitaji kutengeneza maisha yao ya baadaye kwani elimu ni suala la muhimu katika maisha yao.

Mdau wa elimu, Monica Kayanza, alisema pamoja na serikali kuweka mkazo kwa wanafunzi waliochaguliwa kuanza kidato cha kwanza, bado baadhi ya wazazi hawaoni umuhimu huo.

Alisema wazazi wanachangia watoto hao kutoripoti na utoro mwingine kwa kuwa hawachukui hatua yoyote.

Naye Michael Kanyenzi, mkazi wa Sumbawanga, alizitupia lawama serikali za vijiji kwa kutotumia sheria zilizoko kuwabana wazazi ambao watoto wao hawaendi shule, jambo lililochangia kuongezeka kwa hali hiyo.

# Waziri ataka hatua dhidi ya wafanyakazi kampuni za simu wanaotoa siri za wateja

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

WAZIRI wa Katiba na Sheria, George Simbachawene, amewataka watumishi wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kuzichunguza na kuzichukulia hatua baadhi ya kampuni za simu za mkononi na watumishi wake ambao wanatoa taarifa za miamala ya wateja kwa wahalifu wa mitandaoni.

Alitoa agizo hilo wakati akifungua mafunzo ya makosa ya kimtandao kwa mawakili wa serikali na kusema inashangaza kuona baadhi ya wahalifu wa kimtandao kuwa na taarifa za mteja aliyefanya muamala wa simu.

Alisema kuna uwezekano baadhi ya watumishi wa kampuni hizo si waaminifu ambao wamekuwa wakitoa siri za wateja kwa wahalifu na kusabaisha watu wengi kuibiwa fedha zao.

"Inawezekanaje mhalifu akajua kwamba mtu fulani amefanya muamala wa kuhamisha fedha kama si kampuni za simu zinatoa siri? Amejuaje kama fedha imeingia kwa mtu, kwa nini hizi kampuni msizikamate kwa sababu kinamama wengi ndio wanaibiwa," alisema Simbachawene.

Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Sylvester Mwakitalu, alisema baada ya mafunzo hayo wanaimani mawakili wa serikali watafanyakazi kwa weledi katika kushughulikia makosa ya kimtandao na kuondoa malalamiko mengi ya wananchi.

Alisema miongoni mwa changamoto zilizokuwa zinakwamisha uendeshaji wa kesi hizo ni uelewa mdogo kwa baadhi ya mawakili wa serikali jambo ambalo limesababisha malalamiko mengi ambayo yamekuwa yakielekezwa kwao kutokana na vitendo hivyo kuonekana kuongezeka siku hadi siku.

"Kukaa kwetu Morogoro kwa siku hizi kwanza ni gharama kubwa, lakini kama mnavyofahamu tuko wachache tumesimamisha shughuli kule tulikotoka. Kwa hiyo tuyatumie vizuri mafunzo haya ili kuhakikisha mhalifu asione kama kuna njia ya kupita kufanikisha uhalifu wake," alisema.

Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Makosa ya Kimtandao katika Ofisi ya DPP, Monica Mbogo, alisema lengo la kufanya mafunzo hayo ni kuhakikisha waendesha mashtaka wanakuwa na uwezo wa kukabiliana na makosa hayo hasa wakati huu ambao teknolojia imekua.

Alisema Sheria ya Makosa ya Mtandao si mpya lakini kutokana na sababu za kukua kwa teknolojia, mambo mbalimbali yamebadilika ikiwamo uendeshaji wa kesi na ushahidi unaokusanya na kuwasilisha vielelezo mahakamani.



Ofisa Muuguzi Kiongozi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa Mwananyamala, Pendaeli Massay, akitoa somo kuhusu umuhimu wa kutunza afya, katika semina ya Jinsia na Maendeleo (GDSS), iliyoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) Mabibo, mkoani Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Bashe atangaza fursa uwekezaji katika kilimo

**Na Mwandishi Wetu,** DUBAI

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe, amesema Tanzania iko tayari kushirikiana na kampuni kubwa duniani kuwekeza kwenye kilimo ili kukiongeza thamani na kuhakikisha usalama wa chakula kwa miaka mingi ijayo.

Akihutubia kwenye Maonyesho ya Biashara Kimataifa yanayoendelea Dubai (Dubai Expo) juzi, Bashe alibainisha kuwa Tanzania ina ardhi kubwa yenye rutuba kwa uwekezaji wa kilimo huku mazingira ya uwekezaji yakiwa ya kuvutia uwekezaji katika kila aina ya kilimo.

Waziri huyo alisema kuwa kwa sasa nchi inatafuta wawekezaji wa kimkakati ambao watasaidia uwekezaji wenye tija kwa Tanzania na dunia kwa ujumla, hasa ikizingatiwa kuwa kwa miaka ijayo Afrika ndiyo itakuwa chanzo kikubwa cha chakula.

"Tanzania inawapenda na kuwatambua wawekezaji katika sekta zote hasa za kilimo kwa kuwa ni sekta ambayo ipo na itaendelea kuwapo miaka yote kwa kuwa chakula ni kitu muhimu ambacho bado kinahitajika kwa mustakabali wa mwanadamu kuendelea kuishi, labda wanasayansi waje na utaalamu wa kuweka 'chip' mwilini ili mtu akiamka asisikie njaa," alisema Bashe.

Alisema kuwa kutokana na uamuzi wa Rais Samia Suluhu Hassan wa kupunguza riba za benki hadi kufikia kuwa chini ya asilimia 10 kuwavutia wawekezaji zaidi wa ndani na nje ya nchi, ni fursa kubwa kwa wawekezaji hao kujikita kwenye kilimo kwa kuwa mazingira ni rafiki zaidi.

Bashe alisema Tanzania inajulikana kimataifa kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo ina vyeti vya utambulisho wa kimataifa ambavyo vinawawezesha wawekezaji hao kuuza bidhaa kimataifa kutoka Tanzania.

Alisema: "Nchi ina vituo vingi vya utafiti wa kilimo vilivyosambaa kila kona ya nchi na vinafanya utafiti wa aina ya mazao yanayopaswa kulimwa katika eneo husika. Pia nchi ina nguvukazi ya kutosha ya kufanya kazi kwenye mazingira yoyote ya uwekezaji huku pia kukiwa na motisha nyingi kwa ajili ya wawekezaji. Nchi ipo tayari kufanya kazi na wawekezaji katika kilimo hasa ikizingatiwa ardhi ipo ya kutosha."

Alitolea mfano kampuni ya AVOAFRICA ambayo imesafirisha kontena zaidi ya 200 za parachichi kutoka Tanzania huku akibainisha kuwa kwa sasa nchini kilimo ni biashara na siyo sehemu tu ya kujipatia mlo huku akibainisha kuwa Dubai inachukuliwa kati ya sehemu muhimu kwa kuuza mazao ya kilimo kutoka Tanzania.

Bashe alisema katika kilimo cha matunda na mboga Tanzania inasifika kwa kuwa na uwezo wa kuzalisha aina zote za matunda na mboga huku fursa zikiwa nyingi za kuuza ndani na nje ya nchi.

Alisema kuwa mbali na kuwaalika wawekezaji kutoka nje ya nchi, wizara yake inaendelea kuwathamini na kuwaendeleza wakulima wadogo na imeshawawezesha kunufaika na mikopo ya aina mbalimbali kama ilivyo kwa wajasiriamali wengine wadogo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kupanda bei ya gesi tishio kwa mazingira

**BEI** ya gesi mtungi mdogo imepanda kutoka Sh. 20,000 hadi 25,000 huku mtungi wa kati ukitoka Sh. 53,000 hadi 58,000, ambayo hutumiwa sana na watumiaji wa nyumbani.

Baadhi ya wananchi tayari wameacha kutumia nishati hiyo badala yake wamerudi kwenye matumizi ya mkaa, ikiwa ni namna ya kukabiliana na ongezeko la gharama ambazo wanashindwa kuzimudu.

Kipindi cha nyuma bidhaa hiyo ilipatikana kwa bei iliyomwezesha mtu kununua na kutumia, lakini kadiri siku zinavyosonga inazidi kupanda hali inayotishia usalama wa mazingira nchini.

Mara kadhaa serikali imesema kasi ya uharibifu wa mazingira nchini inatisha, huku ikihamasisha upandaji miti na utunzaji mazingira kwa ujumla wake.

Kuna wakati taasisi kama magereza, shule na vyuo vilitakiwa kutumia gesi au nishati mbadala, ili kuachana na matumizi ya kuni kwa kuwa ndiyo ziliongoza kwa uharibifu kutokana na ukweli kuwa huhitaji kuni nyingi.

Licha ya maelekezo hayo utekelezaji ulikuwa mgumu kwa kuwa bei ya nishati hiyo haishikiki, hadi sasa taasisi hizo zinaendelea kutumia kuni, maana yake tani za miti zinazidi kuteketea.

Wazalishaji wa gesi wanasema hawajapandisha bei bali wamebaki kwenye bei elekezi, lakini uhalisia kwenye soko inauzwa bei ya juu, kiasi cha kujiuliza maswali mengi.

Kwa sasa dunia inapaza sauti dhidi ya uharibifu mkubwa wa mazingira unaochochea mabadiliko ya tabianchi, zipo jitihada za ndani na nje kutunza mazingira ambayo ni muhimu kwa viumbe wote.

Unaposafiri barabara kuu majira ya kuanzia saa 12 jioni utaona mifuko ya mkaa ikitoka porini kuja barabarani, muda huo ndiyo wanunuzi na wauzaji hujitokeza kwa kuwa inajulikana hairuhusiwi kuuza mkaa bila kibali.

Kama nishati hii inazidi kupanda hivi kuna hatari kubwa ya jitihada zinazofanywa na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, zisiwe za mafanikio kwa kuwa mti unaokatwa leo kwa ajili ya kuzalisha mkaa itachukua miaka kadhaa kufikia umri wa kuvunwa tena.

Mara kadhaa viongozi wa serikali kwa nyakati tofauti wameeleza mpango wa kupunguza idadi ya wanaotumia mkaa, waelekee kwenye nishati mbadala, sasa nayo inazidi kupanda kiasi cha wengi kushindwa, lakini uhalisia ni tofauti.

Pia, viongozi hao waliwahi kueleza kuwa ujio wa gesi asilia utasaidia wananchi kusambaziwa nyumbani na kutumia kwa bei rahisi, lakini hadi sasa uhalisia wake ni finyu matokeo yake kasi ya kutumia mkaa inaongezeka.

Ni lazima nchi iwe na mikakati ya kukabiliana na uharibifu wa mazingira, lazima wizara na taasisi zake zizungumze lugha moja, kwamba tuone Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Ofisi ya Kamishna wa Nishati Jadidifu, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, TAMISEMI na Wizara ya Maliasili na Utalii zizungumze lugha moja.

Dunia inazungumzia nishati jadidifu au nishati mbadala ambayo haiharibu mazingira, hamasa kubwa ni kuachana na uharibifu wa mazingira ambao ni tishio kubwa duniani hasa ukataji miti na matumizi makubwa ya mkaa ambayo hutoa hewa ukaa na kuharibu tabaka la juu.

Tayari baadhi ya visiwa Zanzibar, Rufiji, Pangani vimemezwa na maji, huku kina cha bahari na Ziwa Tanganyika kikiongezeka kwa kasi kiasi cha wananchi kushindwa kuendelea na uzalishaji.

Kuhamasisha wananchi waache matumizi ya mkaa bila kuwapa njia mbadala haina maana yoyote, bali ni kutwanga maji kwenye kinu jambo ambalo ni hatari kwa uhai wa kila mwanadamu.

Ni muhimu kuyatunza mazingira kwa jitihada kubwa, kuheshimu sheria, kanuni, sera na taratibu zilizopo, isiwe ni nyaraka za kukaa makabatini au kuacha kushughulika na tatizo.

Mathalani, utaona muuza mkaa anashughulikiwa na idara za maliasili kwa kukamata mkaa wake, ilipaswa kuhakikisha gesi inashuka bei kuhamasisha matumizi kwa kuwa hakuna ubishi, hakuna asiyetaka urahisi wa kufanya shughuli zake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Mvua zinazokuja, wananchi tujipange

**MAMLAKA** ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), ilitoa utabiri kwamba kuna mvua kubwa za masika yaliyopitiliza, yanagonga hodi wakati wowote kwenye maeneo yetu, hivyo wananchi tujihadhari.

Kauli hiyo ya wiki kadhaa zilizopita, zilipigiliwa tena msumari jana, ikiwa na msisitizo wa kumaanisha ilichokitahadharisha.

Mtendaji Mkuu wa Wizara ya Afya, ambaye ni Katibu Mkuu akatoa msisitizo maalum wa tahadhari hiyo, huku akizinyooshea kidole mamlaka mbalimbali zinazoguswa moja kwa moja na athari hizo, ikiwamo wasimamizi wa umeme nchini, TANESCO, akiwataka 'wakae mguu sawa' na kinachokuja kutokana na masika hayo yaliyotajwa.

Ni kauli ya serikali inayotolewa huku kuna salamu kadhaa zimeshajionyesha katika mikoa ya Morogoro, Kilimanjaro, na Singida imekwishapata salamu siku chache zilizopita, Dar es Salaam nayo jana ikisalimiwa na mawingu mazito, yalioambatana na mvua za wastani.

Mara nyingi kuna baadhi ya meneo yatapata mvua za kawaida, lakini baadhi yatapata mvua nyingi na kusababisha athari kwa vitu mbalimbali, hasa miundombinu, binadamu na hata mali.

TMA wamemaliza kazi yao ya kuwatangazia Watanzania, sasa inabaki kwa wananchi wenyewe kuchukua hatua kutokana na utabiri huo, huku taasisi husika za kiserikali nazo ni wakati wao wakiwa makini, kufuatilia kinachoendelea.

Mpaka naandika hivi, tayari mvua zimeanza kunyesha. Kwa bahati nzuri zimeanza kunyesha taratibu kwani hatujasikia mahala popote kuripotiwa uharibifu wa mali, miundombinu na hata maafa.

Serikali iliunda chombo hiki, siyo kama lengo lake ni kuwatabiria na kuwatangazia tu wananchi ili wasikie tu basi kama vile kutangaza matokeo ya mpira au michezo mbalimbali. La hasha.

Hata matokeo ya michezo yakitangazwa kuwa watu watafurahia kwa kushangilia na wengine watahuzunika, ila wakijipanga baada ya hapo wanaendaje?

Pesa nyingi zimetumika kuunda chombo hiki, huku kila mwaka kikitengewa bajeti ya uendeshaji, kutokana kodi za wananchi. Yote hayo ni ishara ya serikali kuwapenda na kuwajali wananchi wake.

Kinyume nayo, ingewezekana tu wananchi hawajui kinachoendelea, wanaanza kuona mvua inanyesha bila taarifa, halafu kwa bahati mbaya kama ikiwa kubwa zaidi wanashindwa jinsi gani ya kujiandaa na kujihami.

Kwa maana hiyo, wananchi wameshahabarishwa kuwepo kwa mvua, hivyo kila mmoja afanye ambavyo ataona ni jinsi gani mazingira yanamruhusu kufanya pale alipo, jibu la mwisho iwe kuepuka balaa.

Na ndicho serikali inachokitaka.

Inawezekana kabisa kuwa baadhi ya watu wapo kwenye mikoa au majiji mengine nje ya mkoa au jiji lake analoishi na familia yake kwa sababu mbalimbali za kikazi au kibiashara na ana mpango wa kutaka kusafiri siku hizi mbili tatu.

Anaposikia taarifa hii inamsaidia kuwahi kusafiri kurejea kwenye familia yake, kwani iwapo atasubiri zaidi asiweze kufanya hivyo kwa sababu inawezekana njiani kukawa na uharibifu wa miundombinu, hivyo ikamsaidia kuondoka huko aliko mara moja.

Wapo wanaolima, wengine tayari wameshatayarisha mashamba, wameshapanda au vinginevyo. Lakini huu ndiyo wakati wa kilimo, hivyo akisikia masika yanakuja, anajiandaa sasa na mambo mengine ya kilimo, pia mengineyo ya mahitaji yake.

Kuna wale wanaoishi maeneo ambayo wanajua kabisa kuwa inapokuja mvua ni matatizo.

Wanapotangaziwa kuwa mvua inakuja, wanakuwa tayari kwa lolote litakalotokea. Kabla hata 'haijachanganya' wanajua wafanye nini. Kila mtu ana mbinu yake ya kuhakikisha nyumbani kwake kunakuwa salama, muhimu taarifa zimemfikia.

Kuna wanaoishi mabondeni, ni miongoni mwa wanaoonewa huruma zaidi. Hivyo taarifa hizo ni muhimu sana kwao, kwani zinawafanya kuchukua hatua za haraka kukomboa familia zao.

Wanachotakiwa ni kuhama, wakikimbilia kuliko salama.

Kutokana na kupanuka kwa miji na vijiji, halikadhalika kuna ufinyu wa miundombinu kwa sasa, yote hayo ni vishawishi vya mafuriko, majengo kujaa maji si mabondeni tu, bali balaa linasonga mbali kila penye mazingira rafiki, yanayopiganwa na kina TMA na wadau wenzake na kiserikali, hata asasi huru.

Kwa kuwa nipo Dar es Salaam, nitoe mfano, hata maeneo yetu, imekuwa kawaida hata kando ya barabara hivi sasa nyumba zinajaa maji.



Mwenyekiti wa Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB), Consolata Ngimbwa (wapili kushoto), akiwasili kwenye ufunguzi wa mkutano wa mafunzo kwa makandarasi wazalendo kuhusu usimamizi wa mikataba ya ujenzi unaoendelea mkoani Dodoma jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# STAMICO sasa yakaribisha migodi kuchoronga madini

**Na Romana Mallya**

SHIRIKA la Madini la Taifa (STAMICO), limesema hadi Julai, mwaka huu, litakuwa na mashine 14 za kisasa za uchorongaji wa madini, hivyo linakaribisha migodi kutumia huduma hizo.

Kadhalika, shirika limekaribisha wafanyabiashara wa madini kutumia kiwanda cha kusafisha dhahabu Mwanza, chenye uwezo wa kusafisha kilo 480 kwa siku kwa kiwango cha kimataifa.

Mkurugenzi wa Rasilimali Watu na Utawala wa STAMICO, Deusdedit Magala, ambaye alikuwa akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa shirika hilo, alisema hayo juzi kwenye mkutano wa nne wa kimataifa wa uwekezaji katika sekta ya madini, uliofanyika jijini Dar es Salaam.

Alisema kwa sasa wanafanya uchorongaji wa madini kwa kutumia mashine za kisasa kwenye migodi mikubwa. "Tunakaribisha migodi mikubwa na kati na wachimbaji wadogo waje kutumia huduma hii ya uchorogaji kutoka STAMICO. Kwa upande wa wachimbaji wadogo, tuna vituo vitatu ambavyo vinafanya kazi ya kuchenjua dhababu na tunatarajia kuongeza vituo vingine katika mikoa inayochimba dhahabu," alisema.

Magala alisema shirika linaagiza mashine tano za uchorongaji dhahabu kwa ajili ya wachimbaji wadogo, zinazotumia mafuta kidogo, ili kulisaidia kundi hilo kwenye shughuli zao.

Kuhusu kiwanda cha kusafisha dhahabu cha Mwanza, alisema kwa sasa wanasafisha tu na mwishoni mwa mwezi ujao wataanza kununua dhahabu kwa wingi kwa kiwango chochote.Katika mkutano huo, Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango alizitaka benki na taasisi nyingine za fedha kwa kushirikiana na STAMICO wabuni namna bora zaidi ya kuwawezesha wachimbaji wadogo wapate fursa ya mikopo, serikali ikiendelea kulifanyia kazi suala la kuanzishwa kwa benki maalumu ya madini.

Magala alisema utekelezaji wake umeshaanza na tayari shirika limeshasaini mikataba mitatu na Benki ya CRDB, NMB na KCB.

"Nia ni kuweza kuwawezesha wachimbaji wadogo wakopeshwe kwenye taasisi za fedha, benki nyingi zimekuwa haziwaamini wachimbaji wadogo au yeyote ambaye wanaona hana mgodi mkubwa, STAMICO tumesimama katikati kusaidia akopesheke," alisema.

Alisema wanaendelea kuongea na benki nyingine, ili kuhakikisha mchimbaji mdogo anakopeshwa kupitia STAMICO ambaye ni mlezi wao.

# Watumishi sita wafutwa kazi kwa utoro

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WATUMISHI sita wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, wamefukuzwa kazi kwa utovu wa nidhamu na kutoonekana kwa muda mrefu kwenye vituo vyao vya kazi bila taarifa.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Ngassa Mboje, alitangaza kufukuzwa kazi kwa watumishi hao kwenye kikao cha Baraza la Madiwani juzi, kilichokuwa na lengo la kujadili mienendo ya watumishi hao na kufikia uamuzi huo.

Alisema baraza hilo kwa pamoja limeazimia kuwafukuza kazi watumishi hao ambao wanatoka kwenye idara mbalimbali kutokana na utovu wa nidhamu na kutoonekana kwenye vituo vyao vya kazi.

Mboje aliwataja watumishi waliofukuzwa kazi kuwa ni Dk. Fidelis Mushi kutoka Kituo cha Afya Nindo, Mteknolojia Maabara Kituo cha Afya Salawe, Andrew Mwakisambwe na Mtendaji wa Kijiji cha Bukene, Charles Mayunga.

Aliwataja watumishi wengine kuwa ni Mtendaji wa Kijiji cha Kilimawe, Mercy Kyando, Omary Omary (Kijiji cha Igembya), Robert Mbuti (Kijiji cha Mwabagehu).

"Hatuwezi kuwa na watumishi ambao hawahudhurii kwenye vituo vyao vya kazi kwa muda mrefu wala hakuna taarifa yoyote juu yao. Hili liwe fundisho kwa watumishi wengine mliomba kazi. Fanyeni kazi msilete mzaha," alisema Mboje.

Pia alisema watumishi wengine wawili watakuwa wakikatwa mishahara yao kwa asilimia 15 kwa muda wa miaka mitatu kutokana na mwenendo wao wa kiutumishi kutokuwa mzuri.

# Mganga mbaroni tuhuma mauaji ya msusi aliyetaka kuzindika mil. 9.5/-

**Na Pendo Thomas** KIGOMA

JESHI la Polisi mkoani Kigoma linawashikilia watu wawili akiwamo mganga wa kienyeji kwa tuhuma za mauaji ya mwanamke, mkazi wa Mrusi wilayani Kigoma aliyekwenda kwa mganga kuzindika

Sh. milioni 9.5 za biashara.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kigoma, Kamishna Msaidizi (ACP) James Manyama, alisema mwanamke huyo, Lidya Kamala (42), ambaye ni msusi wa nywele, alitoweka Februari 16 na ndugu zake walitoa taarifa polisi.

Alisema ilipofika juzi, walipata taarifa za Fanuel Jackson (30) ambaye ni dereva pikipiki aliyembeba mara ya mwisho na alipohojiwa alikiri kumpeleka kwa mganga wa kienyeji, Sabinus Hipolito (50) mkazi wa Kigondo wilayani Kasulu.

Manyama alisema baada ya mahojiano ya kina na kibano kutoka kwa jeshi hilo, watuhumiwa hao walikiri kushirikiana kumuuwa mwanamke huyo na kuelekeza sehemu waliko kuwa wamechimba shimo la futi tano.

Baadae Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, walifanikiwa kuutoa mwili huo na Sh. milioni nane zilikutwa kwa mganga huyo wa kienyeji pamoja na simu ya marehemu.

Alisema jeshi hilo linaendelea na upelelezi ili kubaini kama kuna watu wengine zaidi wanaohusika na tukio hilo la mauaji kisha watuhumiwa watapelekwa mahakamani .

"Jeshi la polisi liko imara tutaendelea kuwasaka kokote waliko na kuwachukulia hatua madhubuti za kisheria," alisema Manyama.

## RITA yatengeneza mfumo wa kidigitali

Na Mwandishi Wetu

WAKALA wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) umekamilisha utengenezaji wa mfumo utakaowezesha bodi za wadhamini wa taasisi kusajiliwa kielektroniki popote ziliko bila kufika ofisi za wakala.

Kwa mujibu wa taarifa yao iliyotolewa juzi na Meneja Masoko na Mawasiliano RITA, Josephat Kimaro, kuundwa kwa mfumo huo ni sehemu ya maboresho yenye lengo la kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wananchi hasa walio mbali na miji.

"Mfumo huu wa usajili wa taasisi umeunganishwa katika Mfumo wa E-Huduma ambao unapatikana ndani ya tovuti ya wakala na moja ya faida yake kwa wakala ni kupata taarifa kwa wakati za taasisi zote ilizozisajili.

"Kabla ya mfumo wa kielektroniki, taasisi zilitakiwa kufika ofisi ya makao makuu ya wakala jijini Dar es Salaam kwa ajili ya usajili na kupata huduma nyingine zote za udhamini, hali iliyoleta usumbufu na kuongeza gharama za uendeshaji," alisema.

Kimaro alisema mpaka sasa zaidi ya taasisi 399 zimeshatumia mfumo huo kupata huduma za udhamini na baada ya kuzinduliwa rasmi hivi karibuni.

Alisema matumizi ya mfumo huo yataiwezesha RITA kupata taarifa sahihi za taasisi zake pamoja na kuunganishwa na mifumo ya taasisi zingine zinazohusika na usajili na kuiwezesha serikali kuwa na udhibiti wa majukumu yao kwa mujibu wa malengo yaliyoainishwa katika katiba zao.

"Baada ya kuingia katika mfumo wa E-Huduma, atatakiwa kufungua akaunti ambayo itamwezesha kupata huduma zote anazohitaji pamoja na kupokea mrejesho na taarifa nyingine kuhusu taasisi yake kutoka RITA.

"Pamoja na kujaza fomu za huduma mbalimbali, kupitia mfumo huu mwombaji pia ataweza kuambatanisha nyaraka zote zinazohitajika, kupata ankara ya ada inayotakiwa kulipwa na kuweka taarifa za malipo," alisema.

Aliongeza kuwa kwa mujibu wa Sheria ya Usajili wa Wadhamini Sura ya 318, Toleo la 2002, taasisi zote zinazomiliki mali zinatakiwa kuwa na Bodi za Wadhamini ambayo hupewa mamlaka kisheria kusimamia mali zake kwa niaba ya wengine kwa madhumuni yaliyowekwa na wadhamini hao wanatakiwa kusajiliwa RITA.

"Taasisi zinatakiwa kuleta marejesho kila mwaka kwa kujaza fomu maalumu kuonyesha uwapo na taarifa mbalimbali za wadhamini ambapo kwa muda mrefu taasisi nyingi zimeshindwa kutekeleza jukumu hilo kwa wakati," alisema.

Alitaja huduma nyingine zinazopatikana katika mfumo huo ni kutoa taarifa kuhusu mabadiliko ya jina la taasisi, kutoa taarifa kuhusu mabadiliko ya wadhamini, taarifa ya kubadili anwani ya posta, taarifa ya kubadili katiba, kupata kibali cha kumiliki ardhi, upekuzi wa taarifa za bodi za wadhamini, kuthibitisha nakala ya nyaraka na kupata nakala ya nyaraka zao zilizosajiliwa.

Alisema mfumo wa E Huduma unatoa nafasi kwa wananchi kupata huduma za udhamini na usajili wa vizazi na vifo kielektroniki na hivi karibuni utaingizwa mfumo wa usajili wa ndoa na talaka.

# Tiba mbadala yatajwa kuwaathiri wagonjwa

Romana Mallya

SERIKALI imesema kwa sasa waathirika wa tiba mbadala ni watu wenye magonjwa yasiyoambukiza, kwa kuwa huishi nayo muda mrefu na wanaposikia kuna dawa huwa wa kwanza kuikimbilia.

Mkurugenzi Msaidizi wa Magonjwa Yasiyoambukiza wa Wizara ya Afya, Dk. James Kiologwe, aliyasema hayo jana wakati wa mafunzo ya siku mbili yaliyohusisha wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, kifua kikuu, Dawa za Kulevya na Magonjwa Yasiyoambukiza, wahariri wa vyombo vya habari na watu wanaoishi na magonjwa. Mafunzo hayo ambayo yalishirikisha washiriki 64 yaliandaliwa na Shirikisho la Vyama vya Magonjwa Yasiyoambukiza Tanzania (TANCDA) na Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA) kwa kushirikiana na Wizara ya Afya kupitia Mradi wa RECAP unaosimamiwa pia na Shirika la Afya Duniani (WHO).

Akizungumza katika mafunzo hayo, Dk. Kiologwe, alisema mtu mwenye magonjwa yasiyoambukiza anaposikia kuna tiba mbadala ya ugonjwa alionao, hutamani suluhisho la tatizo lake litokee haraka.

"Kwa hiyo matokeo yake ni kwamba wapo ambao wanaacha tiba za hospitali baada ya kwenda kwenye tiba mbadala, pia tiba mbadala imesababisha baadhi kuchelewa kwenda kupata huduma.

"Kwa mfano, wagonjwa wengi wa saratani huanzia kwenye tiba mbadala mpaka akifike hospitalini Ocean Road anakuwa katika hatua ambayo ugonjwa umekwenda sana," alitahadharisha.

Kwa mujibu wa Dk. Kiologwe, kutokana na hali hiyo wizara pamoja na mambo mengine, inawawajengea uelewa wadau, wanahamasisha watu wabadili mfumo wa maisha yao.

Alibainisha kuwa dawa nyingi zinazotumika zinazotolewa na baadhi ya watu wa tiba mbadala bado hawajajua kiwango cha kutosha kuhusiana na dozi na athari zake."Hapa ndipo Kitengo cha Tiba Mbadala kinaingia kuhakikisha kwamba tiba zinazotolewa zinakuwa zimefanyiwa utafiti wa kutosha," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema tiba mbadala kwao ni muhimu kuwa sehemu ya kampeni yao ya kudhibiti magonjwa yasiyoambukiza. Dk. Kiologwe alisema utafiti wa viashiria vya magonjwa yasiyoambukiza uliofanyika nchini mwaka 2012, unaonyesha watu 26 kati ya 100 wana matatizo ya magonjwa ya shinikizo la juu la damu na tisa kati ya 100 wana kisukari.

Alisema kuwa hadi sasa kuna visa vipya vya magonjwa ya saratani takribani 40,000 kwa mwaka na ongezeko kubwa la magonjwa ya figo yanayohitaji usafishwaji wa damu na upandikizwaji wa figo.

Alisema ongezeko la wagonjwa limeifanya serikali kutumia fedha nyingi kuyatibu.

"Mwaka 2019, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alizindua programu ya taifa ya kuzuia na kudhibiti magonjwa yasiyoambukiza, ili kuongeza chachu ya kupambana nayo.

"Kampeni ya kitaifa ya kubadilisha mtindo wa maisha italenga zaidi kutoa elimu kwa sababu elimu ndiyo njia kubwa itakayoweza kuokoa maisha ya jamii," alisema.

Alibainisha kuwa katika mafunzo hayo washiriki wamefanya uchambuzi wa kisera kuhusiana na masuala ya lishe.

"Baada ya uchambuzi huu wa kisera wadau wanatarajia kutumia uchambuzi na takwimu watakazopata kutengeneza kampeni ya kitaifa ya kubadilisha mtindo wa maisha ili kusaidia kuondoa viashiria na matatizo haya," alisema.

Mwenyekiti wa Chama cha Kisukari Tanzania (TDA) na Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Magonjwa Yasiyoambukiza Tanzania (TANCDA), Prof. Andrew Swai, alisema wadau mbalimbali walianza kufanya utafiti wa magonjwa yasiyoambukiza ili kuona yameenea kwa kiasi gani tangu mwaka 1986.




Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, Abdu Majid Mwanga (kushoto) na Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Kati, Nsozo Mlozi, wakikata utepe kufungua tawi la benki hiyo katika mji mdogo wa Dumila, mkoani Morogoro, pamoja na kukabidhi vifaa vya Shule ya Msingi Kilosa Town na Shule ya Sekondari Lumuma vyenye thamani ya Sh. milioni 10. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yaonya uharibifu misitu

Na Mwandishi Wetu

KATIBU Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Mary Maganga, amesema zinahitajika hatua za haraka katika kudhibiti vitendo vya ukakaji miti kiholela na uharibifu wa misitu.

Amesema uharibifu wa misitu unachangiwa kwa kiasi kikubwa na shughuli zisizo endelevu za binadamu pamoja na athari za mabadiliko ya tabianchi, akitahadharisha hali hiyo isipodhibitiwa, takriban miaka 40 hadi 50 kutoka sasa, nchi itakuwa katika hatari ya kugeuka kuwa jangwa.

Mary aliyasema hayo jana mjini Morogoro alipozindua mradi wa kujenga uwezo wa taasisi ili kupunguza hewa ya ukaa inayosababishwa na ukataji wa miti na uharibifu wa misitu (REDD+).

Alibainisha kuwa ukataji miti na uharibifu wa misitu huchangia mabadiliko ya tabianchi ambao husababisha uzalishaji wa hewa ya ukaa kwa asilimia takriban 20 duniani. Mary alisema kupunguza uzalishaji wa hewa ya ukaa inayotokana na ukataji wa miti na uharibifu wa misitu ni makubaliano ya kimataifa yanayosisitiza kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kupitia kupunguza utoaji wa gesi joto.

Katibu Mkuu aliongeza kuwa Tanzania Bara inakadiriwa kuwa na jumla ya hekta milioni 48.1 za misitu ambayo ni takriban asilimia 55 ya eneo lote na takriban hekta 106,458 za misitu Tanzania Zanzibar ambayo ni takriban asilimia 41 huku akibainisha ukataji miti kwa mwaka Tanzania Bara unakadiriwa kufikia hekta 469,420 na kwa Zanzibar ni hekta 3,149. "Misitu ina faida kubwa katika maisha ya mwanadamu na viumbe wengine, ikiharibiwa husababisha upotevu mkubwa wa bayoanuai na hatari ya kutoweka kwa baadhi ya spishi muhimu za mimea na wanyama. "Kuharibika kwa bayonuai kunakadiriwa kuigharimu serikali wastani wa asilimia tano ya Pato la Taifa kwa mwaka na kunufaisha zaidi jamii za vijijini zinazotegemea mazingira na maliasili kwa maisha yao ya kila siku.

"Misitu hii ni makazi ya viumbe hai na baadhi yake ni vyanzo vya maji vinavyosaidia ustawi wa maisha yetu na maendeleo ya shughuli mbalimbali za kiuchumi nchini," alifafanua. Mary alisema kuna haja kuendeleza uhamasishaji wa jamii kushiriki katika mipango ya kupunguza hewa ya ukaa kwa kupanda na uhifadhi wa misitu ambayo inanyonya hewa hiyo.

Bjern Midthun kutoka Ubalozi wa Norway nchini, alionyesha matumaini yake katika mradi huo na kusema kuwa utasaidia kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Alipongeza Tanzania kwa kushiriki katika mikutano mbalimbali ya kimataifa kuhusu masuala ya mazingira ukiwamo wa COP26 uliofanyika mwaka jana na kusema ni hatua nzuri katika kuhakikisha athari za mabadiliko ya tabianchi zinaondoshwa. Mkurugenzi wa Mazingira Ofisi ya Makamu wa Rais, Dk. Andrew Komba, alisema kasi ya ukataji miti ni kubwa nchini yetu, hivyo mradi huo utasaidia kutafuta nishati mbadala ili kupunguza ukataji miti kwa ajili ya kuni na mkaa.

Dk. Komba alisema pia kilimo kisichoendelevu kinachangia tatizo hilo, hivyo kupitia REDD+ itatafutwa njia bora ya kufanya kilimo bila kufyeka eneo kubwa kwa ajili ya kulima badala yake kutumia eneo dogo kufanya kilimo chenye tija.

# TANESCO kuunganisha umeme waliolipa 27,000/-

**Na Francis Godwin,** IRINGA

SHIRIKA la Umeme (TANESCO) mkoani Iringa limeanzisha operesheni maalumu ya kuwaunganishia umeme wateja 2,170 waliolipia Sh. 27,000 ili kupata huduma hiyo kabla ya gharama mpya za umeme kutangazwa.

Ofisa Uhusiano wa TANESCO Mkoa wa Iringa, Francis Mbwele, alisema jana kuwa operesheni hiyo inafanywa na kikosi kazi kilichoundwa na TANESCO Mkoa wa Iringa kikihusisha watendaji wake kutoka wilaya za Mufindi, Kilolo na Iringa ili wateja wote walioomba huduma ya umeme, wapatiwe kabla ya Machi 31, mwaka huu.

"Tunachokifanya sasa ni kutekeleza agizo la serikali la kuhakikisha kabla ya Machi 31, mwaka huu wateja wote wawe wameunganishiwa umeme na baada ya zoezi hili kumalizika, TANESCO Mkoa wa Iringa imejipanga mteja wake mpya baada ya kukamilisha kujaza fomu, ndani ya wiki mbili atakuwa ameunganishwa na huduma ya umeme," alisema.

Ofisa huyo alisema idadi kubwa ya wateja ambao walikomba umeme iko mjini Iringa na Kihwele ambako TANESCO imepeleka kikosi kazi cha kukamilisha uingizaji wa umeme kwa wateja wake na baada ya kumaliza huko, kikosi hicho kitaelekeza nguvu zake maeneo mengine ili wateja wote wapate huduma hiyo.

Alisema kikwazo kilichokuwa kinakwamisha wateja kuunganishwa umeme kwa wakati ni upatikanaji wa vitendea kazi ambavyo kwa sasa vipo na wana uhakika wa kutekeleza majukumu yao kwa wakati.

Alisema upungufu wa vifaa ulisababishwa na ongezeko kubwa la wateja ambao walijitokeza baada ya gharama ya kuunganishiwa umeme kupunguzwa mjini na vijijini lakini kwa sasa kasi imepungua.

Mbwele aliwataka wananchi wanaohitaji huduma ya umeme, kuendelea kujitokeza kwa kuwa uhakika wa kuunganishiwa umeme ni mkubwa.

Mhandisi Mkuu wa TANESCO Mkoa wa Iringa, Twaha Kisaka, alisema serikali imetoa muda wa kukamilisha kuwaunganishia umeme wananchi waliolipia kwa kuwa kikosi kazi.

Mteja mpya wa TANESCO na mkazi wa Kitwiru, Amina Sanga, alisema kuwa tangu mwaka jana alipohamia katika makazi yake mapya, hakuwa na huduma ya umeme, hivyo kikosi kazi kilichoundwa ni fursa kubwa kwake. Mary Kususange, Mwenyekiti wa Mtaa wa Kitwiru B mjini hapo, mbali ya kuipongeza TANESCO kwa operesheni hiyo, alishauri utekelezaji wake uwe shirikishi kwa wenyeviti wa mitaa ili kuwaonyesha maeneo yenye uhitaji mkubwa wa umeme.

Alisema mtaa wake una maeneo ya pembezoni ambayo wananchi bado hawajafikiwa na nguzo za umeme, hivyo TANESCO waangalie uwezekano wa kupeleka huduma kwa wananchi hao.



Mafundi wa Shirika la Ugavi la Umeme Tanzania (TANESCO), mkoa wa Iringa, wakiwa katika operesheni ya kuwaingizia umeme wateja wapya zaidi ya 2,170 ambao walilipia 27,000/- katika eneo la Kitwiru, Iringa mjini jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

## Madarasa ya UVIKO-19 yapunguza msongamano

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

KUKAMILIKA kwa ujenzi wa madarasa kupitia fedha za mkopo wa kukabiliana na athari za ugonjwa wa UVIKO-19 zilizotolewa mwaka jana, kumepunguza msongamano wa wanafunzi katika shule za sekondari wilayani Kahama mkoani Shinyanga.

Awali wanafunzi walikuwa wakisoma kwa msongamano katika shule za sekondari, hivyo kuwa na mazingira yasiyo rafiki kwa ufundishaji na ujifunzaji.

Mjumbe wa Serikali ya Mtaa wa Malunga katika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Robert Masunga, alibainisha hayo wakati wa harambee ya ujenzi wa msingi wa jengo la utawala katika Shule ya Sekondari Malunga.

Aliipongeza serikali kwa kuwajengea madarasa matatu ambayo tayari yamekamilika.

Mjumbe huyo alisema awali wanafunzi waliokuwa wakifaulu katika kata hiyo, walikuwa wakisoma katika Shule ya Sekondari Kishimba na huko chumba kimoja cha darasa kilikuwa kinatumiwa na wanafunzi 150 ikiwa ni mara tatu ya inavyotakiwa kisera.

Mmoja wa wakazi wa kata hiyo, Beatrice Peter, alisema kukamilika kwa shule hiyo kutawasaidia wazazi kufuatilia kwa ukaribu maendeleo ya watoto hao kimasomo.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Malunga, Omary Abdala, alisema madarasa hayo pamoja na jengo la utawala ambalo ujenzi wake unaendelea, yanatarajiwa kuanza kutumika Aprili mwaka huu.

Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Kata ya Malunga, Kiteleja Kisika, alisema wajumbe wa mkutano mkuu wa chama hicho walikutana na kujadili juu ya kushiriki katika ujenzi huo na kuongeza kuwa tayari wamepata mifuko 60 ya saruji kutoka chama hicho mkoani Shinyanga.

# Maono ya Gavana Ndulu kuendelezwa

**Na Gwamaka Alipipi**

WADHIBITI waandamizi wa sekta ya kifedha kutoka taasisi mbalimbali duniani wameahidi kuendeleza maono ya aliyekuwa Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), marehemu Prof. Benno Ndulu.

Maono hayo ni pamoja na kuwapo biashara huru katika Bara la Afrika (AfCFTA) hususani katika kuendeleza miundombinu ya malipo ya kikanda kwa gharama nafuu na ya haraka.

Viongozi hao wa Benki Kuu za Afrika walitoa kauli hiyo wakati wa mkutano wao wa pamoja walioufanya mtandaoni juzi, wakiadhimisha dira yake (Prof. Ndulu) ya kipekee ya kiuchumi wa Afrika, ikiwa imetimia mwaka mmoja tangu alipofariki dunia mwaka jana.

Akizungumza katika mkutano huo, Gavana wa BoT, Prof. Florens Luoga, alisema: "Leo ni mwaka mmoja tangu tumpoteze shujaa wetu. Msomi mashuhuri, mchumi mahiri wa maendeleo, mwanabenki mwenye maono, mchambuzi wa masuala ya kifedha, mtu mashuhuri na mtu wa vitendo. Huyu ndiye Profesa Benno Joseph Ndulu."

Mkutano huo uliandaliwa na Wataalamu wa Ushauri wa Maendeleo ya Sekta ya Kifedha (FINSYS), ukiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Utafiti wa Masuala ya Kiuchumi Afrika (AERC), Prof. Njuguna Ndung'u. Prof. Ndung'u alisema: "Inapendeza kuona jumuiya mashuhuri ikiungana pamoja kumkumbuka rafiki yetu mkubwa Prof. Ndulu na kuchunguza jinsi ya kuendeleza maono yake."

Mchumi mwandamizi kutoka Uganda, Dk. Louis Kasekende alisema: "Moja ya michango ya kipekee ya Prof. Ndulu ilikuwa kutambua umuhimu wa kuchochea ukuaji kupitia biashara ya kikanda. "Biashara ya ndani ya Afrika inawakilisha asilimia 16.6 tu ya biashara zote za kuvuka mpaka za Afrika, kuongeza hii itakuwa na faida kubwa za kiuchumi kwa Afrika. Aliona maendeleo ya malipo ya mipakani kama sababu moja muhimu katika kuunga mkono dira hii, na akaanzisha maendeleo ya muda mrefu ya miundombinu ya malipo ya Tanzania na kikanda."

Gavana wa Benki ya Hifadhi ya Afrika Kusini, Lesetja Kganyago alisema: "Bara letu ni miongoni mwa mabara yenye malipo ghali zaidi duniani. Mifumo mipya ya malipo ya kuvuka mipaka itahitaji uratibu wa kimataifa na usaidizi wa kisiasa na hii itategemea sana sekta ya umma na ya kibinafsi kushirikiana. Hatuthubutu kushindwa katika jitihada hii".

Mwenyekiti wa zamani wa Baraza la Malipo la Ulaya, Gerard Hartsink, akichangia kuhusu uzoefu wa ulaya katika kuunda Mfumo wa Malipo katika Nchi za Ulaya (SEPA), alisisitiza uongozi thabiti kutoka benki kuu na ushiriki wa sekta kibinafsi.

Pia alisisitiza uwiano wa maendeleo ya kimataifa na mtazamo wa kiafrika wa marehemu Prof. Ndulu.

# Gharama mpya uunganishaji wa umeme zazua mvutano

**Na Julieth Mkireri,** CHALINZE

BARAZA la Madiwani wa Halmashauri ya Chalinze mkoani Pwani limeomba kufanyika marekebisho ya bei za kuunganisha umeme hususani kwenye maeneo ya vijijini kwa kuwa vigezo vinavyotumika haviendani na hali halisi ya maisha ya wananchi.

Wakizungumza kwenye kikao cha Baraza la Madiwani juzi, madiwani hao walisema maeneo yameainishwa wananchi wake walipie kiasi cha Sh. 27,000 na wengine bei mpya ambayo imependekezwa katika kata moja.

Mbunge wa Viti Maalumu (CCM), Subira Mgalu, alisema tafsiri ya kijiji imeelekezwa kufuatwa ile ambayo ipo kwa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), lakini inayotumika kwenye halmashauri hiyo ni tofauti kwa vigezo vya Shirika la Umeme (TANESCO).

"Msimgombanishe Rais, Waziri wa Nishati na wananchi. Tafsiri ya kijiji ifuatwe ile ya TAMISEMI. Sasa hii mnayofanya mnataka wananchi waichukie serikali yao," alionya mbunge huyo.

Subira alisema elimu inahitajika kutolewa kwa wananchi ambao maeneo yao yana uhitaji wa kupatiwa huduma hiyo ili kuondoa sintofahamu.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Bagamoyo, Abdul Sharifu, aliliomba shirika hilo kuzingatia vigezo na masharti wakati wa kuwaunganishia umeme wananchi.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Hassan Mwinyikondo, alisema ni vyema Meneja wa TANESCO Mkoa wa Pwani akafika katika Baraza la Madiwani kuwaelezea utaratibu wanaoutumia sasa kuunganisha umeme katika maeneo ya halmashauri hiyo.

Kaimu Meneja wa TANESCO Wilaya ya Chalinze, Elieza Minja, alisema maeneo ambayo mradi wa REA unaendelea, wananchi wataendelea kutozwa Sh. 27,000 kuunganishiwa na maeneo mengine yameainishwa bei watakazokuwa wanatozwa.

Minja alisema yapo maeneo ambayo hayako mjini lakini kuna vigezo vimeainishwa kwa shirika hilo kutoza bei mpya na kwamba utaratibu wa kuwaunganishia umeme wananchi unaendelea kwa kufuata vigezo.



Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Stephen Kagaigai, akipanda mti kama ishara ya kupokea msaada wa miche asili 2,100 iliyotolewa na Benki ya ABSA Mjini Moshi, juzi. Wengine ni Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Mahusiano wa benki hiyo, Aron Luhanga (aliyechuchumaa kulia), Meneja wa Tawi la Moshi, Pendo Abdallah (kushoto) na Ofisa Mauzo wa benki hiyo, Baraka Haule. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NBC yaja na mfumo mikopo wachimbaji wa madini nchini

**Na Jumanne Juma**

KATIKA kukuza uwekezaji wa Sekta ya Madini nchini, Benki ya Biashara ya Taifa (NBC) iko mbioni kuanzisha mfumo mpya wa ukopeshwaji wa mikopo kwa wachimbaji wa madini.

Mfumo huo unatarajiwa kuondoa vikwazo mbalimbali vya uwekezaji kwa wachimbaji wadogo na wakubwa wa madini nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa Mkutano wa Kimataifa wa Uwekezaji katika Sekta ya Madini Tanzania 2022 jijini Dar es Salaam juzi, Mkurungezi wa Biashara wa NBC, Elvis Ndunguru, alisema kuwa hivi karibuni benki yao itaanzisha utaratibu wa kukopesha wachimbaji wadogo na wakubwa kwa kuweka dhamana ya madini yenyewe.

Ndunguru alisema utaratibu huo utakuwa wa kwanza kuanzishwa na benki yao nchini ambao utampa fursa mchimbaji wa madini kuweka dhamana ya madini yake na kuondoa usumbufu wa dhamana za mikopo.

"Hii ni mara ya kwanza kuanzishwa kwa utaratibu huu nchini na Benki ya NBC ndiyo itakuwa ya kwanza nchini na itawapa fursa wachimbaji wadogo, wakubwa na wasambazaji kupata mkopo kwa urahisi.

"Kufikia mwezi wa sita (Juni) tutakuwa tumeshaanza, mfumo umeshaandaliwa na hivi karibuni tutakuja kuelezea zaidi na namna mchimbaji atafaidika na mkopo kupitia madini anayoyachimba," alisema.

Ndunguru alisema NBC pia imeondoa vikwazo vya mikopo kwa wachimbaji wadogo na wakubwa ambapo kwa sasa wanapata mikopo kwa urahisi zaidi.

"Hata kama kuna mteja anahitaji kupata vifaa vya uchimbaji au magari, kwa sasa kupitia NBC tumerahisisha upatikanaji wa mikopo kwa kuondoa vikwazo vyote ambapo awali vilikuwa vinawafanya wachimbaji wasipate kwa haraka," alisema.

Mnufaika wa NBC, Mwenyekiti wa Industrial Miners Tanzania Group, Judith Sanga, alisema benki hiyo imekuwa na mchango mkubwa kwa Sekta ya Madini hususani kwa upande wao ambao wamerahisisha utaratibu wa mikopo kwa wachimbaji wa madini.

"Kiukweli NBC imekuwa na mchango mkubwa sana, ni benki ya kwanza kutufikia sisi wachimbaji na utaratibu wao ni mzuri na wanakusiliza pale unapokuwa unahitaji msaada wao.

"Wanachokitaka ni vile vigezo ambavyo ni pamoja na leseni ya uchimbaji na mikopo unaipata kwa haraka na tunawashukuru sana," alisifu.

# Wizara kukusanya bil. 221/- za pango

**Na Joseph Mwendapole,** DODOMA

WIZARA ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi mwaka huu imepanga kukusanya Sh. bilioni 221 kutokana na kodi ya pango la ardhi na imeanza kwenda nyumba kwa nyumba kuwatafuta wadaiwa sugu.

Mjini Dodoma jana Mkuu wa Kitengo cha Kodi ya Ardhi, Denis Masami, alibainisha hayo alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu kampeni inayoendelea nchi nzima kukusanya kodi hiyo.

Alisema kutokana na kampeni inayoendelea, mwitikio wa wananchi kulipa kodi hiyo umekuwa mzuri na mpaka sasa wameshakusanya Sh. bilioni 81.2.

Masami alisema wizara hiyo imerahisisha ulipaji wa kodi hiyo ambapo mwananchi anaweza kulipia kupitia simu yake ya kiganjani badala ya kulazimika kwenda benki kufuata huduma hiyo kama zamani.

Alisema moja ya kazi wanayofanya ni kutoa elimu kuhusu umuhimu wa kulipa kodi hiyo kwa njia rafiki kwa kufanya makadirio akiwa nyumbani kwake kwa kutumia mitandao ya simu na kisha kulipa kwa njia hiyo hiyo.

Alisema baadhi ya wananchi wamekuwa wakichanganya kati ya kodi ya pango la ardhi na kodi ya majengo, hivyo wamekuwa wakijitahidi kuwaelimisha wajue tofauti.

"Kodi ya Majengo ni ile inayokusanywa na Mamlaka ya Mapato (TRA) kupitia LUKU na Kodi ya Pango la Ardhi inakusanywa na Wizara ya Ardhi na inakusanywa kupitia mifumo yetu ya kielektroniki, hivyo ninatoa rai kwa wote wanaodaiwa walipe kwa maendeleo ya nchi," alisema.

Aliongeza kuwa mkakati mwingine wa kuhamasisha malipo ya kodi hiyo ni kupita nyumba kwa nyumba kuhakikisha kila kipande cha ardhi kinachodaiwa kinapelekewa, akisisitiza kuwa mpango huo umeonyesha mafanikio makubwa.

Masami alitoa mfano wa mafanikio hayo kuwa katika Jiji la Dodoma ulipaji wa kodi hiyo umeongezeka katika kipindi cha Desemba kwa kuwa ndani ya wiki mbili za kwanza wamiliki 200 walilipa kodi hiyo, lakini baada ya kuanza kuwafuata waliongezeka hadi kufikia 800 kwa wiki.

"Kwa Jiji la Dodoma tu mapato yaliongezeka kutoka Sh. milioni 40 kwa wiki mpaka Sh. milioni 102 kwa wiki moja. Kwa hiyo utaona ongezeko ni kubwa na tuna kituo cha mawasiliano kwa wananchi kinachotoa huduma hiyo," alisema.

Aliongeza kuwa wapo wateja ambao wamekuwa wakiomba kulipa madeni yao kidogo kidogo, hivyo watumishi wa wizara hiyo walioko kwenye kituo hicho wamekuwa wakiwasaidia namna ya kulipa.

"Kama mteja akiahidi kwamba atalipa wiki moja ijayo, mfumo wetu unarekodi na siku hiyo ikifika mfumo unamkumbusha mtumishi wetu kwamba unatakiwa kumhudumia mteja fulani mwenye namba hii ya malipo, sasa mtumishi anawasiliana naye analipa," alisema Masami.




Ukurasa 13

Viberenge mlimani vitatutumbukia nyongo!


BUFE

IJUMAA FEBRUARI 25, 2022

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Nipashe





**MJUE KIJANA LINDA**
**Aonyesha ishara ya kuigwa kujiajiri akibuni 'NGO' yenye mazito mtaani**

Ukurasa 14

# Bodi ya Pamba inavyopambana katika safari ngumu kunasua wakulima wake

**Na Anthony Gervas, Mwanza.**



Mkulima wa pamba akiwajibika. **PICHA: MTANDAO.**

DESEMBA 3 mwaka jana, ndiyo ilikuwa ni tarehe ya msimu wa kilimo cha pamba kimkoa, ulizinduliwa katika kijiji cha Bugatu, kata ya Ng'haya wilayani Magu, mkoani Mwanza na wakulima wakasherehekea sana neema hiyo kuanza.

Balozi wa Bodi ya Pamba Tanzania, Aggrey Mwanri, ndiye aliyezindua msimu kwa kuwakabidhi zawadi za baiskeli wakulima bora wa msimu uliotangulia, ikiwa ni tuzo yao itakayotumika kuwa nyenzo ya usafari wakati wa kwenda shambani kulima au nyakati za mavuno.

Mwanri alizindua pia shamba darasa la mfano katika upandaji mbegu kwa kutumia 'sentimita shimo hadi shimo' na kuzingatia kanuni za kilimo bora cha kisasa, ili kuongeza uzalishaji badala ya kulima kiholela.

Moja ya mambo aliyowapiga marufuku wakulima ni kwamba wasilime pamba kwa kuchanganya na mazao mengine,akisema "yeyote atakayebainika, serikali itamuangalia jicho la dharau, atakamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria."

Pia, kauli ya balozi huyo siku hiyo iliangukia kwenye kilio na maswali ya wakulima kuhusiana na bei kila msimu kulalamikiwa kuwa ni 'kiduchu' mfano mwaka uliopita wa kilimo, 2021, bei ya pamba kilo moja ilikuwa kati ya shilingi 1,150 hadi wastani wa shilingi 1,500 katika maeneo mengi.

Wapo waliokata tamaa kuendelea na kilimo hicho, wakidai hakina tija, badala ya kukua uchumi wao bali unadidimia, ambao wameamua kuacha kulima pamba na kuhamia kilimo cha mazao mengine ya biashara na chakula kama mpunga, alizeti, choroko na dengu.

Yote hayo yanadaiwa yanaakisi kukosekana majibu sahihi kutoka Bodi ya Pamba Tanzania, ambayo ndiyo wasimamizi wakuu wa zao hilo, wakisaidia upatikanaji wa soko zuri duniani, ili mkulima aweze kuuza kwa bei nzuri yenye manufaa kwake na kuondokana na malalamiko ya kila mwaka 'kushuka bei.'

Wakulima wanakuwa wanabeba mzigo mzito kichwani na wamekuwa wakiuliza maswali kipindi sahihi ambacho Bodi ya Pamba itawasaidia kuutua mzigo huo, hata wakanufaika na faida, ili waanze kupatikana mabilionea kupitia dhahabu hiyo nyeupe.

Swali, ni lini wakulima wa pamba watapewa kipaumbele cha bei na kuheshimiwa kama wazalishaji wakubwa wa malighafi hiyo inayozalisha nguo viwandani na mafuta ya kupikia, pia upatikanaji mashudu yatokanayo na mbegu kwa ajili ya shughuli zingine za uzalishaji mali ikiwemo kulishia mifugo.

Hadi sasa mustakabali unaonyesha namna Bodi ya Pamba, ina nafasi ya kuwatua mzigo wakulima kuhusiana na malalamiko ya bei ndogo ya pamba nchini. Majibu ya maswali hayo ya masoko yako mezani kwa asasi hiyo iliyokabidhiwa jukumu.

Inatajwa katika sura ya pili ya shilingi, wanunuzi hudai bei kushuka katika soko la dunia ndio kunachangia, hivyo wananunua bidhaa hizo za shambani kulingana na hali ilivyo sokoni.

Balozi Mwanri anaganda katika msimamo, wa kuwahamasisha kulima kwa bidii, wakizingatia kulima kwa kanuni za ubora ili kuzaa tija na kipato kikubwa mwisho wa safari.

Katika uzinduzi huo, akahimiza kila mkulima awe anaelewa kwa kina yahusuyo upandaji bora wa mbegu na umbali kati ya shimo moja na lingine.

Anahimiza wakulima waondokane na changamoto za umaskini, ili kila mmoja wao anufaike kupitia pamba, ikizingatiwa kilimo ni sekta mama iliyobeba wastani mkubwa wa uchumi wa nchi na maendeleo ya umma, ikibebwa na wadau; wakulima na wafugaji.

Zao pamba bado limebeba nafasi kubwa katika uchumi wa wakulima, hasa katika mikoa ya Kanda ya Ziwa, hivyo linatakiwa kuungwa mkono na kupewa kipaumbele na serikali.

Ndio maana zamani uzalishaji wa mikoa hiyo ya Kanda ya Ziwa, ulichangia ujenzi wa viwanda vingi vya nguo kitaifa, vikiongozwa na Mwatex ya Mwanza, maana ulikuwa ukanda ngome wa kuzalisha malighafi ya nguo.

BIASHARA

## CHANIKAJIJINI DAR; NI KICHEKESHO KULIVYOPEWA JINA...

# Panakua kwa kasi, umati uliopitiliza, biashara juu, majina makubwa kitaifa, msukumo sasa iwe wilaya

**Na Salome Mwasamale**

KATIKA historia inayohusu Jiji la Dar es Salaam, inapogeuziwa kisogo nchi ilikotoka wastani miaka 40 hadi 50, kuna maeneo yaliyojulikana kuwa 'shamba' wakati huo, msamiati huo sasa unaweza kuwa mgumu, pale anapoambiwa mgeni wa anauona mji kwa sasa.

Zama hizo maeneo kama Mbezi wilayani Ubungo na Buza, wilayani Temeke, kulikuwa shamba wakati huo, hali kadhalika Gezaule (Kigambonii) na Tegeta (Kinondoni) kukawa vijiji ambako leo hii, maalum kuhamishia 'wazururaji mjini' kwa mujibu wa sheria ya wakati huo.

Hapo ndipo kitongoji Chanika, nacho kinaingia katika orodha hiyo, kutoka sifa ya kijiji hadi kufika miaka ya 1990, sasa ni mji mpya, unaounda sehemu ya Jiji la Dar es Salaam. Hiyo inaendana na kutapakaa daladala na magari takriban saa 24, umati wa wakazi uko juu, huku baadhi wenye majina makubwa.

Naam huu ndio uhalisia! Hebu pata kibwagizo kimojawapo cha mengineyo; kwamba ilikuwa wikiendi iliyopita tu watu wakijimwaga burudani la dansi palepale mjini Chanika, mara nikamwona mzito mmoja wa kitaifa akiserebuka, kisha akaenda kuwatunza waburudishaji mmoja baada ya mwingine, posho za karatasi zinazofanana na rangi ya 'Msimbazi.'




Sehemu ya barabara kuu inayopatikana Chanika, jijini Dar es Salaam.

**MIAKA 70 ILIYOPITA**

Zinajulikana sehemu nyingi za nchi kumeshuhudiwa mikoa, wilaya, maziwa, mito ikiwa na majina inayoelezwa asili yake lazima inaacha mshangao kama si kichekesho.

Chanika, imo katika kata 36 zinazounda Halmashuri ya Jiji la Dar es Salaam (zamani Manispaa ya Ilala).

Upande wa Mashariki imepakana na kata za Msongola, na magharibi kuna msitu wa Kazimzumbwi, ni kata ya Buyuni na upande wa Kusini iko Zingiziwa.

Kata ya Chanika ina mitaa minane ya kiutawala ambayo ni; Vikongoro, Nguvu Mpya, Ngwale, Tungini, Lukooni, Kidugalo, Yongwe na Virobo.

Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012, Kata ya Chanika ina jumla ya wakazi 43,912 na kaya 11,123, huku Iddi Singirimo (60), mkazi mkongwe wa eneo hilo ana simulizi ya chimbuko lake.

Anaanza na jina Chanika limeanza wastani miaka 70 iliyopita, kutoka kwa wakazi wake, akifafanua wengi wazawa jamii ya Wazaramo, mmoja wao babu yake mzaa baba.

Anasema hapo walikuwa wakisafirisha biashara zao kutoka maeneo ya Maneromango wilayani Kisarawe, kwenda kuuza katika soko la Ilala. Safari yao, ilianzia huko walikotoa bidhaa wanatembea nazo na kulala nazo Chanika na siku inayofuata wakaelekea Ilala sokoni.

Singirimo ambaye sasa ni babu, anasimulia safari ya kilomita 85 iliyochukua siku mbili kutoka makazi aliyoyaita Uzaramoni kupitia Masaki hadi Chanika kunakotimu kilomita 60, kisha kutoka Chanika hadi Ilala ni kilomita 25.

"Wazee wetu wa zamani walikuwa na nguvu sana za kutembea, lakini hawakuwa na nguo za kutosha ili kuweza kujisitiri, hiyo ndiyo ilipelekea chimbuko la jina Chanika," anaeleza.

Anasema, katika kipindi hicho, mmojawapo wa wazee hao waliosafiri, alikuwa na kutumia nguo moja ya 'kuaka nikuvae' pasipo kuibadilisha, hivyo ilifika hatua nguo hiyo ikachakaa na kwa bahati mbaya kuna siku alifika hapo nguo yake ikachanika.

Watu walipokea tendo hilo kwa namna ya mzaha, kukiwapo kundi walilocheka sana na kusimuliana mkasa huo.

Walisikika wakisema 'Vilihi' wakimaanisha vipi? Na kuendelea" kuna munu vyavikile aho anaidipoli yahoo nguo yake Idegeka," wakiwa na maana kuna mtu amefika hapo kwenye pori lake nguo yake imechanika walisimuliana huku wakicheka.

Neno Idegeka inamaanisha 'imechanika; likasambaa eneo kubwa, ndipo kuna watu walipoanza kusimuliana hilo kwa Kiswahili na kujikuta eneo hilo likiitwa Chanika (Degeka).

**VITUO MAJINA YA WATU**

Singirimo, ambaye naye sasa ni babu, anaendeleza ufafanuzi kwamba, wageni wengi huwa wanashangaa eneo la Chanika, vituo vyake vingi vya mabasi vina majina ya watu.

Hili analifafanua kwamba, mizizi wake unatokana na hizo safari za koo mbalimbali za wafanyabiashara walioolazimika kufika katika vituo vyao kila mmoja na sehemu yake na ndio ukawa mzizi wa majina ya vituo.

Hapo inaendana na mifano, vituo vya mabasi vya sasa, vinasikia kwa majina leo kama vile kwa Dadi, kwa Ngwale, Kwa Zoo, kwa Mazinda, kwa Chikira, Kwa Midobe, kwa Dude na Kwa Bandula.

Pia, anataja zipo sehemu kama Nguvukazi, ni eneo ambalo zamani lilikuwa na watu wenye nguvu (watu wa miraba minne) walilazimisha watu kulima, ili wawezeshwe kujipatia chakula.

Eneo la Msumbiji, lenyewe lilikuwa maarufu kwa wasifu zamani waliishi jamii ya Wamakonde, wengi watokao Msumbiji wakiwa na chale usoni, walifikia eneo la hilo wakaishi peke yao.

Pia kuna eneo la Magenge ambako palikuwa mahali pa watu kujinufaisha kibiashara, vilevile kwa ajili ya ushindani wa starehe, kijamii na kifamilia.

**MAGEUZI MAKUBWA LEO**

Hivi sasa kuna ushuhuda namna eneo Chanika kuna ongezeko kubwa la watu, pia kasi ya ujenzi unaifanya shughuli za uchumi kushamiri, kwa maana hata kila kilichopatikana eneo la mjini kama Kariakoo, sasa kinapatikana Chanika.

Doweko Yange (68) ni Ofisa Mtendaji mstaafu wa Kata ya Mkuranga, kwa sasa akiwa mkazi wa Chanika. Anaelezea sababu ya ongezeko linatokana na baadhi ya wenye majina na wadhifa mkubwa kitaifa, kuwekeza Chanika, akiwataja viongozi kadhaa wa ngazi za juu kitaifa.

Anasema hilo limewafanya wananchi wengi nao kuitumia fursa hiyo kuwekeza kwa namna tofauti Chanika, huku akiongeza kuwa operesheni mbalimbali zilizofanywa na serikali kuhamisha watu, ikiwamo upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere, ni sehemu ya yanayochangia ongezeko wakazi Chanika.

"Chanika awali haikuwa na shule, bali ilikuwa na kituo kimoja cha kufuta ujinga kiliitwa Tapa, ambacho kilikuwa Videte," anaeleza kwa mifano hai.

Yange anaendelea: "Sasa hivi kuna stendi ya mabasi, lakini sasa tunajivunia maendeleo makubwa, tuna shule nyingi za awali, msingi na sekondari za serikali na za watu binafsi ni maendeleo makubwa!

"Hatukuwa na huduma za afya, tulikuwa tukitegemea Hospitali ya Amana na Kisarawe (mkoa Pwani), lakini sasa tuna hospitali kubwa ya mama na Mtoto ya Nguvu Kazi, ambayo inatoa huduma zote ikiwamo ya upasuaji, tunamshukuru Mungu na viongozi wetu kwa ujumla," anaeleza Mzee Yange.

Vingine anavyotaja ni vituo vya afya na zahanati ndogo za watu binafsi, pia maduka ya dawa.

**CHANGAMOTO ZILIZOKO**

Kuhusu changamoto, wazee Singirimo na Yange wanaiomba serikali kuipa Chanika hadhi wilaya, ili kufanikisha kutatua changamoto walizo nazo sasa.

Wanataja la kwanza ni kukosekana shule iliyo na kiwango cha kidato cha sita, hali kadhalika Chuo cha Maendeleo ya Ufundi (VETA), huduma za kibenki na kiserikali kuanzia ngazi ya wilaya, nyingi zinapatikana mbali.

Anadokeza katika hilo wengi hawana nguvu za kuzifuata huduma hizo kwa gharama kubwa au umbali mrefu.

"Chanika sasa ina hadhi kabisa ya kuwa wilaya. Tunaiomba serikali ifikirie ombi letu hilo ambalo tayari viongozi wetu wameshalifikisha sehemu husika. Kutoka huku hadi kwenye ofisi za wilaya ni mbali sana, wananchi wanatumia zaidi ya saa mbili kwenye gari kufuata huduma wilayani," anatamka.



Mradi wa majengo ya kiserikali yanayouzwa eneo la Buyuni jirani na mji wa Chanika, Dar es Salaam. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Viberenge mlimani vitatutumbukia nyongo!






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: jkulangwa@yahoo.com

NILIPATA kupendekeza huko nyuma kuhusu utalii wetu nchini, nikaenda mbali kusema ikiwezekana katika ndege zetu kuwe na ugali au uji wa ulezi badala ya kulisha Wazungu chakula cha Wazungu.

Siku nyingine nikapendekeza, ikiwezekana katika mbuga na hifadhi zetu, kukajengwa nyumba za msonge au tembe, Wazungu wakalala humo badala ya kulazwa kwenye maghorofa na majumba ya vioo.

Sikuishia hapo, nikataka kama ikiwezekana, wakaangiwe senene na kumbikumbi wale, ikiwezekana hata panzi na mende, ili waonje chakula cha Kiafrika. Nikataka pia wavae migololi wakiwa vijijini au mashuka ya kimasai.

Sikusikilizwa, naona kila kitu kinakwenda kwa namna yao ya asili, wakati wanapotoka kwao kuja huku kutalii hutarajia kukuta mazingira na vitu na hata tabia za kiafrika, lakini hususan za kitanzania, hivi kweli wanayakuta hayo? La hasha. Hawakuti uji bali chai na gahawa!

Tunafanye sasa, ili kuwaonyesha kuwa tunaishi hivi na hawa wanyama wetu? Hivyo, wakirudi kwao wakasimulie jinsi walivyokuta Watanzania wakiishi na wanyama hao, badala ya kufikiria kuhamisha Wamasai walikokuwa wakiishi na wanyama wakali.

Hebu fikiria kabla hili la binadamu na wanyama, halijatulia hivi sasa tumesikia tena tuliyosikia, yale ya miaka miwili iliyopita, ya kutaka kufunga viberenge vinavyoning'inia kuelekea Kilimanjaro mlimani, eti kwa ajili ya watalii.

Hivi kweli unawekaje kiberenge Mlima Kilimanjaro ili Watalii wafike kileleni kwa kuning'inia? Hebu tuwe makini kidogo na hili jamani. Hivi mnataka kuacha zile njia zetu za Horombo kweli? Mnataka fumba fumbua mtu yuko kileleni!

Tukae chini tufikirie upya kuhusu viberenge hivi kama vitatusaidia. Mjue viberenge viko huko ughaibinu na wanavitumia sana kwa mambo yao ya kutoka sehemu moja kwenda nyingine. Sisi tunataka kuacha utaratibu wa zamani wa kutembea siku kadhaa mpaka kufika kileleni kweli!

Hivi hamjui hiyo tembea ya kukwea mlima ni burudani kwa watalii? Hivi mnadhani mkiweka viberenge vyenu hivyo watakuja tena? Wanafurahia sana kutembea na kuona mazingira, huku wakiimbiwa na ndege na kunyeshewa kidogo na manyunyu ya mvua, huku wakikatakata matawi ya miti njiani. Nyie mnatafuta viberenge!

Hivi hamjui kuwa watalii wakiwa njiani kwenda mlimani, yaani kileleni, wanafurahia kukaa kwenye vituo na kufurahia kula na kunywa na kuona wadudu na ndege warukao? Mnataka viberenge ili iweje, wataviona wapi hivyo? Watapiga picha gani wakaoneshe kuwa tulipita hapa na pale?

Hamtaki pia kufikiria kuwa kufungafunga minyaya humo kwenye njia zinazoelekea kileleni mtaharibu mazingira ya mlima huo mtukufu? Yote hayo mbona yalipata kusemwa miaka miwili iliyopita, mmesahau mara tu? Au kuna jambo linapikwa?

Haya angalieni, mkiweka viberenge mjue wale machalii wetu wanaosindikiza watalii watakosa ajira, sasa mtawapeleka wapi? Kila siku tunalia ajira hakuna, vijana wanamaliza vyuo vikuu wanakosa ajira na wengine kujiweka humo sasa mnataka kuwatemesha tena!

Ni bahati mbaya mnaoamua hamjui haya, watoto wa walalahoi wanaojikimu kwa kusindikiza wapanda Mlima mnataka kuwakatili kwa viberenge!

Niliposema watalii waje kula ugali kwenye ndege, au kulala kwenye nyumba za msonge na tembe au kumtafuna senene na kumbikumbi, nilikuwa namaanisha uhalisia wa maisha, kwamba wakija hao wageni wajifunze maisha halisi ya Watanzania ambayo si ya viberenge bali kutembea, yaani kukwea mlima kwa miguu.

Tusikimbilie kubadili utalii wetu kuwa bandia, kwa kuanza kuingiza vitu ambavyo vitaharibu uhalisia huu. Kumbukeni, jirani anachungulia kuona jinsi tutakavyokosea kwa kuingia huko kwa viberenge, basi wao watawavuta wakiwambia huku tunapanda kwa miguu na kujionea uhalisia wa nchi.

Yaani mnataka watu sasa watumie dakika 20 kufika kileleni na 10 kurudi, badala ya siku tano au sita na 10 za kusoma mazingira kweli? Hivyo mtalii akija kwa siku moja anakuwa amemaliza kila kitu na kulala siku moja na kuondoka. Hayo mapato mtatoa wapi? Nini faida ya utalii? Alamsiki!

UCHUMI

MJUE KIJANA LINDA

# Aonyesha ishara ya kuigwa kujiajiri akibuni 'NGO' yenye mazito mtaani

Na Maulid Mmbaga

KILIO cha serikali sasa ni vijana wengi kitaifa wanaolia kukosa ajira. Hivyo, katika kupunguza makali ya tatizo hilo, viongozi wengi serikalini na nje ya serikali, wamekuwa wakisisitiza mbadala wa kujiajiri baada ya kuhitimu masomo.

Hata hivyo, wako vijana wanaodai wanakwama baada ya kukumbana na changamoto, pia upatikanaji mtaji wa kuanzisha biashara za kuwawezesha wasukume maisha yao.

Wazo pingamizi dhidi ya hilo, wanadai ni fikra ya uvivu, kwani wapo vijana wanaofanyia kazi ushauri hata wanajikwamua kutoka kwenye umasikini.



Mkurugenzi wa Taasisi ya Nolimit Foundation, Linda Bonson, ( wa pili kutoka kulia) akifurahia jambo na watoto wenye ulemavu wa ngozi, baada ya kuwapatia msaada wa pedi. Wa kwanza kushoto ni mlezi wa watoto hao, Florida Frank. **PICHA ZOTE: MAULID MMBAGA.**

**SIMULIZI YA MFANO**

Hapo ndipo anapopatikana kijana Linda Bonson, mkazi wa Kurasini, Manispaa ya Temeke, alikofanikiwa kuanzisha kampuni ya mavazi ya 77 Clock na taasisi ya Nolimit Foundation, inayojikita katika kutoa elimu na kuwasaidia wenye uhitaji, pia makundi maalumu kama walemavu, wazee, yatima na wasiojiweza. Pia, inajihusisha na utoaji elimu, wakizama zaidi katika uelimishaji masuala ya afya.

Anasema tangu kuanzishwa taasisi hiyo, wamefanikiwa kutoa elimu na misaada katika shule mbalimbali, akitaja mifano Shule ya Msingi Mivinjeni na Sekondari, Miburani.

Maeneo mengine anakohudumia ni vituo vya watoto yatima anavyovitaja jina la Salvation Army na Kisarawe, katika baadhi ya makazi wamekuwa na lengo la kuwafikia wasiojiweza na kuwaelimisha, ili kuwaongezea uelewa.

"Tunapoenda kutoa msaada na elimu, wale tunawachukulia kama familia zetu, tunaweka utaratibu wa kuwafuatilia maendeleo yao.

"Pia, suala la hedhi tumeona ni tatizo kwa wanafunzi wa kike, hivyo katika baadhi ya shule tumeweka masanduku kwa ajili ya kuhifadhi taulo (pedi) zitakazokuwa zikiwasaidia wanafunzi kujisitiri pale watakapokuwa na uhitaji.

"Hilo tumeliweka katika utaratibu maalum, kwamba mwanafunzi atakapojiona kuwa anakaribia hali hiyo, anaenda kumuona mwalimu mkuu (au mkuu wa shule) sanduku liko pale, anapatiwa pedi anajisitiri anaenda kuendelea na masomo kama kawaida. Hivyo, hawezi kuwa na sababu nyingine ya kutohudhuria masomo," anaeleza Linda.

Anafafanua, elimu wanayoitoa inalenga kuielimisha jamii kutambua ulemavu sio sababu, akifafanua baadhi wamekata tamaa kwa kuuvaa ulemavu na wanajiona hawamudu chochote, akiwaletea mbadala wa wanachokiweza.

Kiongozi huyo wa asasi isiyo ya kiserikali, anasema kuna watoto wenye uwezo wa kiakili, lakini wanaishi katika mazingira magumu hata kufikia hatua kushindwa kuendelea na masomo, kwa kukosa uwezeshaji.

"Nakumbuka kwa mara ya kwanza nilipoanzisha hii taasisi, nilipata nafasi ya kumtembelea mama mmoja ambaye ni (single parent) ana watoto, lakini mazingira yake yalikuwa hayaridhishi.

"Tulifanikiwa kumuwezesha kuanzisha biashara ambayo inamsaidia kukidhi mahitaji ya watoto na kuhudumia familia kwa ujumla. Tunategemea kuendelea kuwasaidia watanzania zaidi kwani wenye uhitaji ni wengi na ukisema uchukue labda wanawake tu, hiyo itaonekana unatenga wengine.

"Mimi siwezi kusema naenda kumuangalia mama, halafu namuacha mtoto wake, hicho kitu hapana! Tunaishi katika mazingira ambayo kila binadamu lazima tupendane," anasema Linda.

**WITO KWA VIJANA**

Linda anatoa wito kwa vijana kuwa na uthubutu utakaowasaidia kuendesha maisha yao, akidai kabla hawajafanya chochote wajitambue uwezo wao na anawasisitizia watu kuepuka kufanya chochote ili mradi wana uelewa, muhimu ni kukifanyia utafiti.

"Kabla hujafanya biashara, lazima ujue unataka kufanya nini (what is your passion), moyo wako unakutuma kufanya nini, usifanye biashara kwa sababu tu ni biashara.

"Unapaswa ujue unafanya biashara gani, unaelekea wapi, unatafuta nini, malengo yako ni nini na jitihada zako unazielekeza kwenye nini? Kutoka akilini mwako kwanza, lazima uwe umejiandaa vya kutosha, ujitambue mimi ni mtu wa aina gani nataka nifanye nini," anaeleza.

Linda anaendelea: "usikimbilie biashara kwa sababu ni biashara 'passion' (utashi) yako 'mindset' (fikra) yako imekaa vipi? Hivyo ni muhimu kuvizingatia kwani wengi wanakimbilia biashara lakini wanafeli, changamoto ni nyingi mno."

Upande wake anasema kajifunza hulka ya kuwa na uthubutu na kutokata tamaa, akitoa angalizo ni vibaya kufanya jambo kwa kuiga, kwa kuwa changamoto haziko katika upande wa ajira tu, bali kwingi.

**MZIZI WA 'NGO'**

Linda anasema, vituo vya kusaidia wasiojiweza ni vingi, vikubwa na vinajulikana, mitaani kuna watoto wengi hawajulikani serikalini, jambo lililomsukuma kuanzisha taasisi hiyo kuwaibua watambulike na mamlaka.

Katika orodha hiyo ya wasiojulikana, anasema, wapo wasiokuwa na usimamizi maalum, hivyo timu yake imejitolea kuzunguka katika maeneo tofauti kutafiti na kutambua makundi yaliyoko.

"Tumeamua tuanze kwanza kwetu na Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, imetupatia kibali cha kuhudumia Temeke nzima na shule zote. Nolimit Foundation (taasisi yake) tunaamini katika upendo, kuwafikia wasiojiweza na waliokata tamaa na kuwawezesha," anasema Linda.

**NENO LA WANUFAIKA**

Mwanafunzi mnufaika wa msaada unaotolewa na taasisi hiyo, akiwamo Frank Godfrey, kutoka Shule ya Sekondari Kurasini mwenye tatizo la uono na usikivu hafifu, akiwa yatima anakiri msaada wa vifaa mbalimbali vitakavyo muwezesha kuendelea na masomo, ni vya muhimu.

"Naishukuru sana (Nolimit Foundation) kwa kunitia moyo, kuubadilisha muonekano wangu na kuniwezesha kuweza kuendelea na masomo yangu kama kawaida, lakini bado nahitaji msaada zaidi.

"Katika matokeo yangu ya kidato cha pili kwenda cha tatu nilipata division 1.7. Pia nawashukuru walimu wangu kwa jitihada zinazonifanya niendelee kufanya vizuri katika masomo yangu," anasema Godfrey.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mgulani, Shukrani Majula, anasema wanachokifanya taasisi hiyo kuwasaidia katika utoaji elimu ni la manufaa, kwamba inaleta motisha kwa wanafunzi na wazazi hata waweze kuhamasika na mazingira mazuri ya watoto wao.

"Watu wajitoe na waige hawa wenye nia njema ya kuwasaidia watoto wenye uhitaji, hasa huku katika shule, kwani tukiwasaidia hawa watoto na kuwawekea mazingira mazuri, inasaidia hata kuongeza kiwango cha ufaulu," anashauri Majula.

Mlezi katika kituo cha kulelea watoto wenye uhitaji cha Kisarawe Ophanage Florida Frank, anasema wako walemavu, yatima, wasiojiweza na waliotelekezwa na wazazi, akibainisha kwamba wanakabiliwa na changamoto mbalimbali, ikiwamo kukosa fedha za kuwasomesha baadhi ya watoto ngazi ya elimu za juu.

Pia anaishukuru asasi ya Nolimit, kujitoa kuwasaidia chakula na kukidhi baadhi ya mahitaji yanayotoa moyo na upendo kwa watoto wanaowasimamia.




Mkurugenzi wa taasisi ya Nolimit Foundation, Linda Bonson (wa kwanza kushoto) akimkabidhi mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Kurasini Frank Godfrey, vifaa vya kumsaidia katika masomo yake ikiwemo madaftari, viatu, yunifomu, begi na viatu vya michezo.





# RC ashangaa halmashauri kutegemea ushuru choo kama chanzo cha mapato

**Na Paul Mabeja,** MPWAPWA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, amemtaka Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa kutafuta vyanzo vya mapato vya kudumu badala ya kuendelea kutegemea ushuru wa vyoo.

Mtaka alitoa agizo hilo juzi wilayani hapo alipofanya ziara ya kukagua utekelezaji wa maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan ya uwekaji wa anwani za makazi.

Alisema viongozi wa wilaya hiyo wanatakiwa kuwa wabunifu katika kutafuta vyanzo vya mapato vya kudumu badala ya kuendelea kutegemea ushuru wa vyoo kama sehemu ya chanzo cha kudumu.

"Lazima mfanye 'transformation' (mabadiliko) katika suala la ukusanyaji wa mapato badala ya kuendelea kutegemea ushuru wa vyoo. Halmashauri kama hii ni aibu kuomba watu wajisaidie ili upate mapato, vipi kama hawatajisaidia utajiendeshaje," alisema Mtaka.

Pia alimtaka kuanzisha miradi ya kimkakati ambayo itaongeza mapato ya halmashauri ili kujiendesha.

"Mpwapwa mnataka kuwa Manispaa lakini hamwezi kufikia huko kama mtaendelea na 'spirit' (mwendo) hii (huu). Lazima mbadilike, hata huu ushuru wa mazao ambao ndio mnautegemea na unaongoza katika ukusanyaji wa mapato lazima muangalie namna ya kufanya kwani kama leo serikali itafuta ushuru huo hamtafikia malengo yenu," alisema Mtaka.

Kuhusu maagizo ya Rais Samia juu ya utekelezaji wa mpango wa anwani za makazi aliyoyatoa jijini Dodoma, Mtaka alisema kila mtumishi anatakiwa kutimiza wajibu wake kukamilisha kazi hiyo kabla ya muda uliotolewa na serikali.

"Maagizo haya Rais aliyatoa katika mkoa wetu wa Dodoma na sisi tulikuwapo, hivyo itakuwa aibu sana kama leo hii mtu wa wilaya kama ya Katavi huko akakamilisha mapema kabla yetu wakati yeye maagizo yale kayaona kupitia televisheni lakini sisi tulikuwapo ana kwa ana na Rais," alisisitiza Mtaka.

Kadhalika, aliwataka mwenyekiti wa halmashauri hiyo pamoja na mkurugenzi kutokuwa kikwazo cha kukwamisha utekelezaji wa mpango huo.

"Rais ndiyo mwenye fedha za kutekeleza mpango huu hivyo basi alishatoa maagizo kuwa kama kutakuwa na mahitaji ya fedha za ziada kuongezeka halmashauri lazima zitoe kwa wakati kufanikisha mpango huu wa makazi," alisema Mtaka.

Kuhusu elimu, Mtaka alisema wilaya hiyo bado inayo kazi ya kufanya katika kuongeza ufaulu wa wanafunzi wa madarasa ya mitihani.

"Mpwapwa lazima muwe wabunifu katika kuboresha ufaulu wa wanafunzi kutengeneza timu ya taaluma ambayo itakuwa na mikakati katika matokeo yenu wilaya nzima yenye majimbo mawili ya uchaguzi mnao wanafunzi 43 tu waliopata ufaulu wa daraja la kwanza yaani Shule ya St. Francis matokeo yake yameizidi wilaya nzima," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Mwanahamis Ally, alisema atahakikisha anayasimamia na kuyatekeleza kwa maslahi ya wilaya na wananchi wake maagizo yote yalitotolewa.

"Kweli mimi sina muda mrefu hapa lakini mkuu wa mkoa tayari kuna baadhi ya mambo nimeshaanza kuyafanyia kazi na nakuahidi kuwa utakaporudi utakuta kila ambacho umeagiza tumekifanyia kazi," alisema Ally.



Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabiri Shekimweri, akiongoza zoezi la upandaji miti katika kata ya Mtumba, jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Machinga kicheko mikopo bil. 200/- za NMB

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

UMOJA wa wafanyabiashara wadogo, maarufu machinga, umesema Sh. bilioni 200 zilizotengwa na Benki ya NMB kwa ajili yao zitasaidia kukuza mitaji na kuwaondoa kwenye umaskini.

Mwenyekiti wa Machinga, Ernest Matondo, aliyasema hayo juzi kwenye mkutano wa wafanyabiashara hao unaendelea jijini hapo ambao umejumuisha viongozi wa machinga kutoka mikoa yote Tanzania Bara, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Makundi Maalum na Jeshi la Polisi.

Matondo alisema kutengwa kwa fedha hizo kumewapa faraja kubwa na tumaini kuwa sasa wanakwenda kuacha kuitwa machinga badala yake wanatengeneza utajiri.

Alisema kwa muda mrefu walikuwa wakiishi kama njiwa asiye na kiota hata mara kadhaa walipotaka kufanya mikutano walishindwa kufanya kwa kuwa hawakuwa na fedha lakini wamepata mtu wa kuwashika mkono.

"Kwa niaba ya wenzangu nasema asante sana serikali, lakini shukrani zangu ziwaendee NMB. Kuna wakati tulifanya mkutano kidogo tuishie kwenda jela, lakini hata mkutano huu wamefadhili wao na mambo yanakwenda vizuri, amani kwa kila mtu," alisema Matondo.

Akizungumza nje ya mkutano, Ofisa wa NMB, Martine Massawe, alisema benki hiyo imeanzisha utaratibu wa namna bora ya kuwainua wamachinga nchini huku akisisitiza kuwa miaka mitano itakuwa ya ukombozi kwao.

Massawe alisema wameingia mkataba na wafanyabiashara hao kwa kushirikiana na serikali ambapo Sh. bilioni 200 zimetengwa kwa ajili ya yao na zitatolewa kwa mpangilio mzuri wa ushirikishwaji ili wasijipenyeze wasiostahili.

Kwa mujibu wa Massawe, kutakuwa na akaunti maalumu kwa ajili yao na wameweka utaratibu ambao utakuwa ukiwatambulisha kila tawi watakalokwenda ili wasiingie kwenye foleni ya kuwachelewesha.

"Si hilo tu, lakini tumewaletea mambo mazuri ikiwamo hata bima ya fao ambapo mtu atakata kwa Sh. 10,000 kwa mwaka, lakini inapotokea tatizo anaweza kulipwa hadi Sh. 500,000 yote hayo tunalenga kuwakuza," alisema Massawe.

Alisema nia ya NMB ni kuona machinga wakibadilika na kukua kutoka hali ya chini kwenda kipato cha kati hadi kikubwa ambapo nao watafikia kuitwa matajili kwa kuwa hata wenye fedha walianzia chini.

Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Zainab Chaula, aliwataka machinga nchini kote kutumia fursa ambayo imetolewa na benki ikiwamo NMB ili kukuza mitaji yao na kuachana na biashara za kukimbizana.

## Bahi na mikakati ufaulu mitihani

**Na Augusta Njoji,** BAHI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Bahi imeweka mikakati 23 ya kuinua kiwango cha ufaulu kwa shule za sekondari na msingi mwaka huu ikiwamo kufanya vikao vya tathmini kila mwezi ili kubaini vikwazo vilivyoko na kuvitafutia ufumbuzi.

Akizungumza jana wilayani hapa katika hafla ya utoaji tuzo kwa shule, walimu na wanafunzi waliofanya vizuri katika mtihani wa kumaliza elimu ya msingi na sekondari 2021, Ofisa Elimu Sekondari wa Wilaya hiyo, Marry Chakupewa, alisema mkakati uliopo ni kuongeza kiwango cha ufaulu kwa kidato cha nne kutoka asilimia 94 hadi asilimia 98 na kidato cha pili kutoka asilimia 96 hadi asilimia 100.

"Tunahimiza pia ufundishaji wa vipindi vya ziada shuleni hasa kwa madarasa ya mitihani kwa kuhakikisha kila shule inakuwa na ratiba rekebishi na kufanya vikao na wazazi mwezi Januari kwa ajili ya kuweka mpango wa kuwapatia wanafunzi chakula cha mchana shuleni," alisema.

Kuhusu kukabiliana na tatizo la mimba, alisema ni vyema watuhumiwa wanaofikishwa kwenye vyombo vya sheria uchunguzi ufanyike haraka na hukumu yao itolewe mapema ili iwe fundisho kwa wengine.

"Tunapendekeza pia wazazi wanaoshawishi watoto wao kufanya vibaya kwenye mitihani yao ya mwisho, kuwazuia wasiende shule au kuwatorosha wachukuliwe hatua ili iwe fundisho lenye lengo la kukomesha tabia hii kwani linaathiri ufaulu licha ya kazi nzuri ya kuwaandaa inayofanywa na walimu," alisisitiza.

Kwa pande wa elimu msingi, Ofisa Elimu Msingi wa Wilaya hiyo, Boniface Wilson, alisema wameweka mikakati 20 ikiwa ni pamoja na wanafunzi kupewa mitihani na kutosha na tathmini ya kina kwa kila somo ili kubaini mapungufu, kupanda na kushuka kwa ufaulu na kubaini masomo ambayo wanafunzi hawafanyi vizuri.

Alisema kwa darasa la saba kuanzia Desemba 2021 hadi Machi 2022, mitihani ya wilaya itafanyika mara moja kwa mwezi na kuanzia Aprili 2022 hadi Juni 2022 mitihani itafanyika mara mbili kwa mwezi.

Alisema kila mitihani inayofanyika ngazi ya kata na wilaya tathmini ifanyike kujua A na B wamepata asilimia ngapi, A hadi C wamepata asilimia ngapi ili kuona mwenendo wa ufaulu na kwa masomo ambayo yataonyesha ufaulu wa chini, walimu wa masomo husika wabadilishe au watafutiwe mbinu ya kuwasaidia.



# DC Mfune atoa siku saba wanafunzi kuripoti shule

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

KUTOKANA na kusuasua kwa kasi ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza kuripoti shuleni katika Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, Mkuu wa Wilaya hiyo, Reuben Mfune, ametoa siku saba kwa wanafunzi hao kuwa wameshafika shuleni.

Mfune alitangaza uamuzi huo jana kwenye mkutano wa hadhara katika Kata ya Luhanga, eneo ambalo lina idadi kubwa ya wanafunzi ambao hawajaripoti shuleni kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo tangazo la serikali namba 28 kulitambua eneo hilo kwamba liko ndani ya Hifadhi ya Taifa Ruaha.

Mfune aliwataka wazazi wote ambao watoto wao wamefaulu kuingia kidato cha kwanza katika kata hiyo, kuwapeleka kwenye Shule ya Sekondari Utengule Usangu kutokana na ujenzi wa shule yao kutokamilika.

Alisema licha ya shule hiyo kutokamilika, pia inasubiriwa hatma ya mgogoro wa mpaka kati ya Hifadhi ya Taifa Ruaha na baadhi ya vijiji vilivyoko Wilaya ya Mbarali.

"Wanaosema watoto wao wataandikishwa kwenye shule ambayo bado haijakamilika wala kusajiliwa, wanapotosha wengine, tuache kudanganywa na watu wanaozungumza vitu ambavyo havina uhalisia," alisema Mfune.

Kiongozi huyo alionya kuwa mzazi yeyote atakayebainika kuweka mgomo baridi na kutompeleka mwanawe shuleni, hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake kwa kuwa kitendo hicho kinamnyima mtoto haki yake ya msingi ya kupata elimu.

Mfune aliongeza kwamba, baadhi ya watu ambao wanawachangisha fedha wananchi na kuwadanganya ni kwa ajili ya kushughulikia tatizo la mpaka wakati linashughulikiwa na ngazi za juu, akisema lengo la watu hao ni kula fedha zao.

Baadhi ya wananchi waliohudhuria mkutano huo, waliiomba serikali kuwasaidia kuharakisha kutoa majibu ya mgogoro huo ili kuendelea na shughuli zao za maendeleo ikiwamo ujenzi wa shule na zahanati.



Mstahiki Meya wa Jiji la Mbeya, Dormohammad Issa, akizungumza na waandishi wa habari, jijini humo jana, kuhusu ujio wa Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, ambapo Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Mbeya mjini, kimeandaa hafla ya kumpongeza kwa kuchaguliwa kushika nasafi hiyo. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## Wajipanga mapokezi Spika mpya wa Bunge

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WANACHAMA wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Mbeya Mjini wameanza maandalizi ya kumpokea Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, ambaye anatarajiwa kuwasili jijini humo mwishoni mwa wiki hii, ikiwa ni mara ya kwanza tangu achaguliwe kushika wadhifa huo. Akizungumza jana na wanahabari jijini Mbeya katika Ofisi cha Chama cha Mapinduzi CCM wilaya hiyo, Katibu Mwenezi wa chama hicho, Philemon Mng'ong'o, alisema tayari wameanza maandalizi ya kumpokea Spika Tulia, ikiwamo kuhamasisha wananchi kujitokeza kwa wingi.

Alisema mbunge wao ameleta heshima kubwa kwa Mkoa wa Mbeya, hivyo lazima mapokezi yake yawe makubwa huku wananchi kutoka maeneo mbalimbali wakitarajiwa kushiriki hafla itakayofanyika kwenye viwanja vya Ruanda Nzovwe jijini Mbeya. "Tunayo furaha kubwa sana kuwaalika wananchi kutoka maeneo mbalimbali ya Jiji la Mbeya kumpokea Spika wa Bunge, Dk. Tulia, ambaye kwa mara ya kwanza tangu achaguliwe kwa kishindo na wabunge wa Tanzania anakuja nyumbani kwao.

"Siku hii ni ya kihistoria, tutasherehekea pamoja ushindi wa kiongozi wetu ambaye ni Mbunge wa Mbeya mjini," alisema Mng'ong'o.

Mstahiki Meya wa Jiji la Mbeya, Dourmohammad Issa, alimshukuru Mwenyekiti wa CCM Taifa, Rais Samia Suluhu Hassan pamoja na uongozi wa chama hicho kwa kupitisha jina la Dk. Tulia kuwania kiti cha Spika wa Bunge.

Alisema wataendelea kumuunga mkono Spika Dk. Tulia katika majukumu yake ya kuwaletea maendeleo wananchi.

## CCM yatangaza kushtaki wazazi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya kimesema kitawafikisha kwenye vyombo vya sheria wazazi na walezi watakaobainika kuwafungia watoto wenye ulemavu ndani na kuwakosesha haki yao ya msingi, ikiwamo kupata elimu na ushiriki kwenye Sensa ya Watu na Makazi Agosti mwaka huu.

Mwenyekiti wa CCM mkoani hapa, Mchungaji Jacob Mwakasole, aliyasema hayo jana alipozungumza na Nipashe kuhusu nafasi ya chama katika kuhamasisha wananchi kushiriki mchakato wa upatikanaji anwani za makazi na sensa.

Mchungaji Mwakasole alisema tayari serikali imetoa maelekezo kwa ngazi za kata na vijiji kuhakikisha wanapita kutoa elimu kwa jamii hususan wazazi wenye watoto wenye ulemavu, kuwafichua hadharani ili kuhesabiwa.

"Kupata mtoto mwenye ulemavu sio mkosi, bali ni thawabu kutoka kwa Mwenyezi Mungu, kumficha ndani ni dhambi kwani nao ni binadamu, wanapaswa kupata stahiki zote kama binadamu wengine.

Nawasihi wazazi wawe waadilifu na waaminifu mbele za Mungu," alisema.

Akizungumzia kuhusu watendaji ambao watapewa dhamana la kuhesabu watu, mchungaji huyo alisema kiapo ambacho watapewa ikiwamo uaminifu, asiwapo hata mmoja ambaye atakwenda kinyume, akionya kuwa kufanya ni kulikosea taifa.

Alisema CCM Mkoa wa Mbeya imejipanga kushirikiana na serikali kuhakikisha Sensa ya Watu na Makazi inawafikia watu wote, yakiwamo makundi maalumu.

Mwenyekiti huyo alisema wataendelea kufuatilia utekelezaji wa maagizo hayo juu ya uandikishaji wa watu wenye ulemavu ili rekodi zao zichukuliwe kwa lengo la kupatiwa huduma mbalimbali kulingana na mahitaji yao.

Katibu Mwenezi wa CCM Mkoa wa Mbeya, Bashiru Madodi, alisema viongozi wa mashina wahakikishe watu wenye ulemavu wote wanatolewa ndani na kuhesabiwa.

"Chama kwa utaratibu wetu huwa kunakuwa na maelekezo maalumu kutoka makao makuu. Tunachofanya sasa ni kunahamisha viongozi wa mashina, tunaamini hawa ndiyo wanaishi na watu na kujua wa mahitaji gani, hivyo wahakikishe wanasimamia hili kikamilifu," alisema Madodi.



# Waziri asisitiza maadili sekta ya afya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wanawake na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, amesema sekta ya afya inasimamia misingi ya heshima, utu, usiri na maadili katika kazi.

Kutokana na hali hiyo, amesema uvunjifu wa nidhamu katika taaluma hiyo ni tabia inayojitokeza kwa baadhi ya watendaji wasiofuata maadili.

Waziri huyo aliyasema hayo jana katika kikao cha Bazara la Wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Nungwi, Abdalla Abass Wadi, aliyetaka kujua ni lini tatizo la wagonjwa kusumbuliwa na baadhi ya watoa huduma katika Hospitali ya Kivunge.

Mazrui alisema uongozi wa hospitali na wizara haujapokea malalamiko kama hayo kutoka kwa wananchi au kikundi cha watu kupitia njia zilizoko katika Hospitali ya Kivunge ikiwamo visanduku vya maoni na namba za simu za viongozi zilizoko kwenye kuta za hospitali au kumwona kiongozi moja kwa moja.

"Mheshimiwa Spika, tunapenda kuchukua nafasi hii kutoa wito na kuwaomba wananchi kuwa mtu yeyote aliyepata au atakayepata hali kama hiyo atoe taarifa kwa uongozi husika wa hospitali au wizara haraka kwa njia zilizoainishwa ili hatua za kinidhamu zichukuliwe. Aidha, wizara itawachukulia hatua kali wale wote watakaobainika kutenda makosa hayo," alisema.

Pia alisema uongozi wa wizara kwa kushirikiana na Hospitali ya Kivunge unaahidi kwamba utaendelea kutoa huduma kwa kufuata misingi ya sheria na maadili ya kazi katika kutoa huduma kwa wananchi ili kufikia malengo ya serikali kwa kutoa huduma bora za afya kwa kuzingatia misingi ya haki, uadilifu na usawa kwa wananchi wote.

Aidha, akijibu swali la Mwakilishi wa Micheweni, Shamata Shaame Khamis, alisema serikali inatambua athari za ugonjwa wa kisukari na wagonjwa wamekuwa wakihudumiwa kupitia kliniki zilizoko katika hospitali mbalimbali. "Naomba ieleweke kuwa ugonjwa wa kisukari ni ugonjwa wa muda mrefu na mara tu mtu anapopata ugonjwa huu anatakiwa afuate taratibu na maelekezo anayopatiwa na wataalamu wa afya," alisema.

Alisema mtu aliyepata ugonjwa huo anaweza kuishi maisha ya kawaida ikiwa atafuata maelekezo ya wataalamu.

Pia alisema serikali inawataka wagonjwa waache dhana ya kurogwa juu ya ugonjwa huo na waache kukimbilia kwa waganga wa kienyeji jambo ambalo linasababisha kuchelewesha kupata matibabu.

Waziri huyo alieleza kuwa madaktari wa kutibu ugonjwa wa kisukari katika Hospitali ya Micheweni wapo na wanatoa huduma pia madaktari hao wamehitimu masomo ya udaktari sambamba na kupatiwa elimu ili kutoa huduma za uhakika.

Mazrui alikri kuna upungufu wa dawa kwa wagonjwa wa kisukari na hakuna wodi maalum ya wagonjwa wa aina hiyo, licha ya ongezeko la wagonjwa na takwimu zilizoko hazijalazimisha kuanzisha wodi maalum.

## Bilioni 111/- zapatikana mauzo ya karafuu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SHIRIKA la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC) limenunua karafuu tani 8,497.82 kwa thamani ya Sh. bilioni 110.89 hadi kufikia Februari 3, mwaka huu.

Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shaaban, aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Kiwani, Mussa Foum Mussa, aliyetaka kujua wizara imeshanunua tani ngapi za karafu na kiasi gani kimeuzwa kwa msimu huu wa mwaka 2021/22.

Waziri huyo alisema mauzo ya karafuu yaliyofanywa ni tani 7,996.61 kwa thamani ya dola za Kimarekani 57,004,854.87 sawa na Sh. bilioni 131.11.

Alisema shirika limefanya mauzo ya mafuta ya mimea yenye thamani ya Sh. milioni 96, mauzo hayo ni kwa ujazo mdogo katika soko la ndani.

Aidha, alisema shirika limekamilisha ukarabati wa kiwanda kwa kubadilisha vifaa kwa ajili ya uzalishaji wa mafuta ili kuuza nje ya nchi.

**Waziri huyo alisema mauzo ya karafuu yaliyofanywa ni tani 7,996.61 kwa thamani ya dola za Kimarekani 57,004,854.87 sawa na Sh. bilioni 131.11.**



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah (wanne kushoto mstari wa mbele), akiwa pamoja Wajumbe wa Kamati ya Maadili na Kinga ya Baraza la Wawakilishi na Wajumbe wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, baada ya kufika katika ofisi za baraza hilo, mjini Zanzibar jana, kwa ajili ya kujifunza. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Wizara yakana michango wazee

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali ZANZIBAR imesema haijaidhinisha mchango wowote kutoka kwa wazee kuchangia uendeshaji wa shule na mzee anapoamua mwenyewe kwa hiari yake kuchangia haikatazwi ila wizara imezuia shule kuchangisha wazee.

Waziri wa Wizara hiyo, Simai Muhammed Said, alisema jana wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Pandani, Prof. Omar Fakih Hamad, aliyetaka kujua kama serikali imeidhinisha michango kwa ajili ya mambo ya serikali kama vile karatasi za ofisi, mihuri, mitihani ya majaribio na bendera ya taifa, ili shule zijiendeshe.

Waziri Simai alisema utekelezaji wa sera ya elimu bila malipo unaendelea kwa shule zote za serikali katika ngazi ya elimu ya lazima.

Alisema serikali inalipia gharama za mitihani ya taifa kwa wanafunzi wote kuanzia ngazi ya elimu ya msingi, sekondari kidato cha pili, cha nne na cha sita.

"Mheshimiwa Spika, msimamo wa serikali ni kuendelea kuhudumia shule zote za serikali za msingi na sekondari bila kuwalazimisha wazee kuchangia hasa kwa wanafunzi katika ngazi ya elimu ya lazima.

"Kwa sasa shule zote za sekondari zinapatiwa fedha taslimu kulingana na idadi ya wanafunzi walioandikishwa katika shule husika kwa kiwango cha Sh.32,000 kwa mwanafunzi kwa mwaka," alisema Simai.

Alisema kiwango hicho ni kikubwa kulinganisha na kiwango ambacho wazee walikuwa wakichangia kabla ya mwaka 2015, ilipofutwa michango hiyo yote. Mzee alikuwa akichangia Sh. 7,000 kwa mwaka.

Aidha, alisema wizara kwa sasa inaendelea na matayarisho ya kuzipatia ruzuku shule za msingi kwa kufanya utafiti maalum wa kuangalia hoja ya kufanya hivyo au kuendelea kuzihudumia kama ilivyo sasa.

Hata hivyo, alisema wizara yake imekamilisha sera mpya ya elimu kutokana na marekebisho ya sera ya mwaka 2006 na kwa sasa wizara inajitayarisha kuipeleka sera hiyo serikalini ili kupata baraka na kuanza matayarisho ya utekelezaji wake ikiwamo matayarisho ya sheria mpya itakayosaidia utekelezaji wake.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**

**Kituo cha JUMUISHI mkoa DAR ES SALAAM**

**Usimamizi wa mirathi na 334/2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU JUMA HAMIS KIROBOTO**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA SAIDI HAMIS KIROBOTO**

**TANGAZO**

**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi mahakama za mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 7 mwezi 3 mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa\ nmsimamizi wa mirathi hiyo
Zingatia,endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa
Imetolewa leo tarehe 15/2/2022

---

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MASJALA YA WILAYA YA MWANZA**
**ILIYOPO MWANZA**

**MAOMBI YA MAREJESHO NO. 19 YA 2021**

**PUNUNTAS COMPANY LIMITED .........MLETA MAOMBI**

**DHIDI**

**EMMANUEL MANONI.............................MJIBU MAOMBI**

**KWA: EMMANUEL MANONI**
**Popote Ulipo**

**KUITWA SHAURINI**

Fahamu kwamba, Shauri tatwa hapo juu ambalo wewe ni mjibu MAOMBI shauri limepangwa kusikilizwa mbele ya Mahakama hii tarehe 23/03/2022 saa 3:00 asubuhi.
Hivyo unatakiwa kuhudhuria Mahakamani wewe mwenyewe au mwaklilishi wako siku hiyo bila kukosa.
Kutohudhuria kwako kutaifanya Mahakama hii iendelee na shauri hili bila wewe kuwepo.
Imetolewa kwa amri na muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 25 mwezi wa PILI,2022.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MWANZA.

---

## KUPOTEA KADI YA GARI

TANZANIA NATIONAL PARKS inatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili SU39252 – LANDROVER DEFENDER. ENGINE NO. 120317064815DT224. CHASIS NO. SALLDHRR7CA421070. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: ARU/ARU/RB/75567/2022

---

## TAARIFA YA KUFUGA KAMPUNI

**MPUKWIN COMPANY LIMITED,** Tunapenda kuutarifu umma kuwa Bodi ya wakurungezi inatangaza kufunga kwa kampuni ya **MPUKWIN COMPANY LIMITED** yenye usajili No. **138926575** yenye makao makuu yake mkoani morogoro kuanzia tarehe 23/02/2022
kwa maelezo zaidi tupigie simu no **0756519090 au 0754319090**

---

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO 23 OF 2022**

**In the Matter of the Estate of the Late THADELY JOHN LONGUKAMA**

**By 1. JOHN JOHN CHOGA**
**2. ......................................**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above – named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 10 day of MARCH...2022

Dated at Morogoro this 17 day of FEBRUARY..2022

RESIDENT MAGISTRATE

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**MASUMBUKO LUPILYA LAZIMA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 588 DDR** YENYE ENGINE NO **21919476** NA CHASISS NO **IBRSPJB56M9016771.** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI **GEI/MBO /RB/ 66340/2022.**

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**QASSM KARAMA JEIZAN** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA DYANA** yenye namba za usajili **T321 AGJ** yenye ENGINE NAMBA **3L3748093** na CHASIS NAMBA **LY6100610065185.** kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa Polisi :-
**KUL/RB/845/2022**

---

## KUPOTEA KADI YA GARI

MARTIN YESAYA MWAKALINGA ANATANGAZA kupotelewa na kadi ya GARI (TOYOTA HILUX) mali ya HARAKA AGENCIES TANZANIA LTD yenye namba za usajili T 176 BSP
Chassis namba: JTFDP626400033205
Injini namba: 2L060775
Kadi Namba: 6180826
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi
taarifa ya polisi RB namba IRI/IRI/RB/79295/2022.

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**FELISTER ELIZABETH GALLATIN** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA KLUGER YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 486 DDG** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI
TAARIFA YA POLISI
**KAH /RB/ 103/2022**

---

## KUPOTEA KADI YA GARI

DICKSON VINCENT MASAWE anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA RAV 4 yenye USAJILI NAMBA T803 DDR, CHASIS NAMBA SXA110173468, yenye ENGINE NAMBA 3S2433665. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:-
ARU/ARU/RB/63426/2022

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**ILIYOPO MOROGORO**

**TANGAZO KUITWA SHAURINI**

**SHAURI LA MADAI NAMBA: 6....2022**

**MDAI: TINGETINGE SACCOS**

**DHIDI YA**

**MDAIWA: ADISTELLA KAINYINGI**

**Kwa: : ADISTELLA KAINYINGI**

**Ombi la mdai: TINGETINGE SACCOS ( KARUME MWISHEHE)**

**Madai ya : SHILLINGI LAKI SITA NA ELFU KUMI NA NANE TASLIM 618000/=**

Unatakiwa kuhudhuria hapa Mahakamani katika shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikiliwa mnamo tarehe 9 mwezi 03 mwaka 2022 saa2:30 asubuhi.
Angalia kama hukuhudhuria/hamkuhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama itathibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa Shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 24 mwezi 02 mwaka 2022.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya DODOMA**

**Kituo cha DODOMA MJINI Mkoa DODOMA**

**Shauri la Madai/Ndoa Na.18/2022**

**Jina la Mdai DENIS BEATUS**

**Jina la Mdaiwa AGATHA MICHAEL**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba (maelezo ya madai) Naomba mahakama ivunje ndoa kati ya mimi na mdaiwa kwa sababu amukuwa hana uaminifu katika ndoa nimemkamata akiwa na meseji za kimapenzi za bwana huyo. Hivyo naomba tuachane.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 11/03/2022 saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinazohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**Angalizo:** kama hakuhudhiria siku ilitajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 23/02/2022.

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE & ADMINISTRATION CAUSE NO.......**
**2021**
**In the matter of the estate of the late MMOTI SIMON SAMBAY of Chinoje Area within Dodoma Region.**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY RAHABU SIMON SAMBAY**
**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN 369 OF 163)**

All PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 25 Day of 02,2022
**Date at Dodoma this 10th Day of December,2021**

RESIDENT MAGISTRATE

---

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

# NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Putin aanzisha vita rasmi, Ukraine yajibu haiogopi



Mwanamama akisubiri usafiri wa treni kuondoka mjini Kyiv, nchini Ukraine, jana. Majeshi ya Russia yanadaiwa kuivamia Ukraine huku milio ya milipuko ikisikika miji ya Kyiv, Kharkiv na Odesa. **PICHA: AP**

**Kyiv,** UKRAINE

NI taarifa rasmi sasa inayotawala pembe zote za dunia, kwamba tangu juzi, Russia imeamuru majeshi yake kuvamia Ukraine kwa vikosi vyake vikitumia njia tofauti za ardhini, anga na baharini.

Wakati kuna hatua hiyo, Ukraine iliyoahidiwa kukingiwa kifua na Marekani, Rais wake Volodymyr Zelensky, amemjibu mpinzani wake Rais Vladimir Putin wa Russia, kwamba haiogopi lolote na kila raia wake ataingia vitani kukabili uvamizi huo.

Reuters, imeripoti kusikika kwa milio ya makombora mjini Kyiv, dakika chache baada ya Rais wa Russia, Vladimir Putin kuamuru kutuma wanajeshi, Mashariki mwa Ukraine, akidai kitendo hicho ni kuwalinda raia wakiwamo Warussia.

Watu saba wanaaminiwa kufariki katika shambulio la bomu lililofanywa na vikosi vya Urusi, Polisi wa Ukraine wanasema.

Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky amesema kuwa atampatia silaha mtu yeyote anayetaka, kulingana na shirika la habari la kitaifa la nchi hiyo, akidai haiogopi chochote wala mtu yeyote.

Inakadiriwa kuwa idadi ya wanajeshi wa Russia, ndani na karibu na Ukraine inaweza kuwa kati ya 100,000 na 190,000 katika wiki za hivi karibuni.

Jeshi la Ukraine, ni dogo zaidi kuliko lile la Russia, ingawa linapata usaidizi kutoka kwa Jumuiya ya Kujihami ya Nchi za Magharibi (NATO).

Marekani haijatuma wanajeshi wowote nchini Ukraine, lakini imetuma wanajeshi 3,000 zaidi nchini Poland na Romania, ili kuimarisha vikosi vya NATO na imewaweka wanajeshi wengine 8,500 katika hali ya tahadhari.

Ijumaa wiki iliyopita, Marekani ilisema Russia, imetuma wanajeshi kati ya 169,000 na 190,000 ndani na karibu na Ukraine.

Michael Carpenter, balozi wa Marekani katika Shirika la Usalama na Ushirikiano la Ulaya (OSCE), anasema: Idadi hii inajumuisha wanajeshi walioko karibu na mpaka na Ukraine, na Belarus, na katika Crimea inayokaliwa.

Wakati huo huo, Waziri wa Ulinzi wa Uingereza, Ben Wallace alisema kuwa asilimia 60 ya wanajeshi wa Jeshi la Urusi wako karibu na mpaka wa Russia na Belarus.

Putin, anasema jeshi lake linakwenda huko kulinda amani ingawa Marekani inaitaja hatua hiyo kama 'upuuzi'.

Russia, ilikuwa imetuma wanajeshi wapatao 200,000 kwenye mpaka wa Ukraine kwa muda wa miezi kadhaa awali.

Jeshi la Russia, lina mizinga na silaha zingine katika mkusanyiko huu, pia wanapata msaada wa jeshi la anga na la wanamaji.

**UKRAINE, RUSSIA NINI CHANZO?**

Mvutano kati ya Ukraine na Russia, ni wa miaka mingi, licha ya juhudi za kidiplomasia katika kutafuta suluhisho la mzozo huo.

Yapo masuala kadhaa, yaliyopo nyuma ya mzozo huo yakiwamo nchi na eneo zima.

Russia, ilitwaa eneo la Crimea mwaka 2014, ikisema ina madai ya kihistoria kwa peninsula hiyo. Ukraine ilikuwa sehemu ya Umoja wa Kisovieti (USSR).

Putin anakumbuka kuanguka kwa Umoja wa Kisovieti mwaka 1991 kama 'mgawanyiko wa Urusi ya kihistoria'.

Katika makala ndefu mwaka jana, aliwaita Warusi na Waukraine "wa utaifa sawa". Wataalamu wanaamini kwamba hii inaonesha mawazo ya Putin. Katika makala hiyo, Putin pia alisema kuwa kiongozi wa sasa wa Ukraine anaendesha "mradi dhidi ya Urusi".

Russia, pia imekasirishwa na kutotimizwa kwa makubaliano ya amani ya Minsk ya 2015 kwa mzozo wa Mashariki mwa Ukraine.

Hadi sasa hakuna makubaliano yaliyofikiwa ya ufuatiliaji huru wa uchaguzi katika maeneo mengine zaidi ya Bara. Russia, imekuwa ikikanusha madai kuwa yote hayo ni sehemu ya mzozo mrefu.

Hivi karibuni nchi hizo mbili, chanzo cha mgogoro kilianza baada ya kuwekwa ulinzi mkubwa wa jeshi la Russia, na kupeleka vikosi vyake kwenye mpaka wa Ukraine.

Ushahidi umerekodiwa na picha za satellite huku zikifichua kuwapo kwa wanajeshi takribani 100,000 eneo hilo.

Wizara ya Ulinzi ya Russia, ilitoa picha za vikosi vyake vikifanya luteka, wakiwa na vifaa kama vile bunduki za kujiendesha, mizinga ya vita na magari ya mapigano.

Kutokana na hali hiyo, Ukraine iliingia wasiwasi juu ya majeshi hayo ya Russia kuwa karibu na mpaka wake, ingawa serikali ya Ukraine ilidai haiamini kama Russia, bado iko katika nafasi ya kuchukua hatua za kijeshi.

Mara kadhaa Russia, ilidai luteka isiwe tishio kwa Ukraine na ikisema yenyewe ina haki ya kufanya chochote inachotaka na jeshi lake ndani ya eneo lake.

Wachambuzi wa siasa za kimataifa wanasema huenda Russia ilijiandaa kulipeleka jeshi kubwa zaidi Ukraine, tangu Vita Baridi.

Mara kadhaa, imesema haina mpango wa vita, ingawa mwaka wa 2014 ilitwaa rasi ya Crimea, Kusini mwa Ukraine na kuwaunga mkono waasi wanaoiunga mkono Russia, walioteka sehemu kubwa za mashariki mwa Ukraine, ilikadiriwa zaidi ya watu 14,000 walifariki, zaidi ya 33,000 walijeruhiwa.

**ATHARI MGOGORO**

Bei ya mafuta na gesi ilianza kupanda wiki hii, baada ya hofu ya mzozo wa Ukraine na Russia, ambao umetatiza usambazaji kote duniani.

Bei ya mafuta yasiyosafishwa imepanda zaidi ya dola 99 (£73) kwa pipa, baada ya Rais Putin kuagiza wanajeshi kuingia Mashariki mwa Ukraine.

Uamuzi wa Russia, kuivamia Ukraine tayari umesababisha bei ya mafuta kupanda na bila shaka itasababisha kupanda kwa bei ya mafuta hadi pauni 1.50 kwa lita ya petroli isiyo na risasi, msemaji wa kampuni ya mafuta ya RAC, Simon Williams, anasema.

Sehemu kubwa ya mafuta na gesi ambayo Uingereza inaagiza haitoki Russia, ila itaathiriwa na kupanda kwa bei ya kimataifa. Bei ya wastani ya dizeli Uingereza ilifikia paundi 152.51 kwa lita siku ya Jumatatu, chini ya rekodi ya Jumapili wiki iliyopita ikiuzwa paundi 152.58.

"Utegemezi wa kiuchumi kati ya Russia na Ulaya, huenda ukazuia hatua za Magharibi kuendelea," Shaistah Akhtar, mtaalamu wa sheria za vikwazo kutoka kampuni ya sheria ya Uingereza Mishcon de Reya, anasema.

**WASULUHISHI KIMATAIFA**

Licha ya nchi za Magharibi kuongeza vikwazo vipya vya kimataifa dhidi ya Russia huku Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Guterres akimsihi Putin kuchagua amani badala ya vita wakati wa kikao cha dharura kuhusu Ukraine, juzi usiku, kwenye Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa jijini New York Marekani.

Waziri Mkuu wa Pakistan, Imran Khan amewasili Russia juzi, kwa mkutano na Rais Putin. Khan, ndie kiongozi wa kwanza wa kigeni kuzuru Moscow tangu Putin kutambua uhuru wa Jamhuri zilizojitenga na Ukraine za Donetsk na Luhansk.

Maofisa wanasema viongozi hao wawili watatathmini uhusiano wa nchi hizo mbili pamoja na ushirikiano wa nishati.

Viongozi hao wawili walijadili masuala ya kikanda ikihusisha maendeleo ya Asia kusini. Safari hiyo ni ya kwanza kwa Waziri Mkuu wa Pakistan kwenda Russia, tangu mwaka 1999.

***Imeandaliwa na Christina Mwakangale kwa msaada wa mtandao***

HABARI MICHEZO

# FEI TOTO AUONA UBINGWA MSIMU HUU UKITUA YANGA

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya timu yake kupata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Mtibwa Sugar, kiungo nyota wa Yanga, Feisal Salum 'Fei Toto' amesema msimu huu lazima waubebe ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara pamoja na Kombe la FA.

Akizungumza na gazeti hili , Fei Toto alisema siri ya wao kufanya vizuri katika michezo yao ni kumsikiliza kocha wao kwa umakini pamoja na kufuata maelekezo anayowapa nje na ndani ya uwanja.

"Msimu huu tunataka kubeba ubingwa ndio maana tunajitahidi kupata ushindi katika kila mchezo," alisema Fei Toto.

Kiungo huyo alisema hata hivyo timu yao itakutana na changamoto mbalimbali katika kila mechi kwa sababu timu zote zimejipanga kuonyesha ushindani kwenye mbio hizo za kuwania ubingwa.

Akizungumzia mchezo dhidi ya Mtibwa Sugar ambao walifanikiwa kuchukua pointi tatu muhimu alisema ulikuwa mgumu na wenye ushindani kwa dakika zote.

"Mchezo ulikuwa mgumu na wenye ushindani, Mtibwa ni timu bora, lakini sisi tulifuata vizuri maelekezo ya kocha tukafanikiwa kutoka na pointi tatu," Fei Toto alisema.

Aliongeza anawashukuru wachezaji wenzake kwa kupambana katika mechi hiyo ya ugenini na kuahidi wamejipanga kuendeleza ushindani kwenye mchezo unaofuata wa ligi hiyo inayotoa mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Matokeo ya juzi yameifanya Yanga kufikisha pointi 39 na kuendelea kujiimarisha katika kilele cha msimamo wa ligi hiyo ambayo imemaliza mzunguko wa kwanza.

Yanga pia imeweka rekodi ya kuwa timu pekee ambayo haijapoteza mechi kwenye mzunguko huo wa kwanza huku Mtibwa Sugar ikiendelea kudidimia kwa kubakia na pointi 12, ikikaa nafasi ya 15 kwenye msimamo huo wenye timu 16.

Mabingwa watetezi wa ligi hiyo ni Simba ambao wana pointi 31 na wako katika nafasi ya pili kwenye msimamo huku Tanzania Prisons yenye pointi 11 ikiburuza mkia.



Naibu Waziri wa Wizara ya Sanaa, Utamaduni na Michezo, Paulina Gekul (katikati aliyekaa), akiwa pamoja na viongozi wa Chama cha Mpira wa Miguu cha Wanawake Tanzania (TWFA) na Chama cha Netiboli nchini (CHANETA), baada ya kikao cha kujadili maendeleo ya michezo hiyo juzi jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Simba Queens waenda likizo

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Simba Queens umesema umevunja kambi ya timu yao inayoshiriki Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania ili kupisha kalenda ya kimataifa inayoendelea ambapo Timu ya Taifa ya vijana wa umri chini ya miaka 17 inajiandaa kuikaribisha Botswana.

Wachezaji wa Simba Queens ambao ndio mabingwa watetezi wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, wamepewa mapumziko ya muda wa wiki mbili.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa Simba Queens, Selemani Makanya, alisema baada ya mapumziko hayo, wachezaji watarejea kuendelea na maandalizi ya mechi za mzunguko wa pili wa ligi hiyo.

Makanya alisema anaamini timu yao itaendelea kuonyesha makali yake kwa kupata matokeo chanya na hatimaye kutimiza malengo waliyojiwekea.

"Tutarejea na nguvu mpya kwa ajili ya kuhakikisha tunaendelea pale tulipoishia, lengo letu msimu huu pia ni kufanya vizuri, likizo hii inatokana na baadhi ya wachezaji kuitwa kwenye majukumu ya timu zao za taifa," alisema Makanya.

Aliongeza wanawapongeza wachezaji kwa kufanikisha malengo ya awali ya kumaliza mzunguko wa kwanza bila kupoteza mechi.

Simba Queens inaongoza ligi hiyo ikiwa na pointi 33 baada ya kushinda mechi zote 11.

## Mastraika, mabeki Prisons kunolewa

**Na SaadaAkida**

ILI kuinusuru na janga ya kushuka daraja, Kocha Mkuu wa Tanzania Prisons, Patrick Odhiambo, amesema ameendelea kuisuka upya timu yake kuanzia katika safu ya ulinzi na kuimarisha idara ya ushambuliaji kwa ajili ya kufanya vizuri katika mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Bara unaotarajiwa kuanza leo, imefahamika.

Tanzania Prisons inaburuza mkia katika msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa na pointi 11 baada ya kucheza mechi 15 wakati Yanga yenye pointi 39 iko kileleni.

Odhiambo amekiri kikosi chake hakipo sawa hivyo anapambana kukibadilisha na kukiimarisha katika kila idara kwa lengo kupata mabadiliko ya uchezaji.

Alisema ana imani baada ya kufanyia kazi maeneo hayo mawili, watarejea katika mzunguko wa pili wakiwa tofauti na hatimaye kurejesha matumaini ya kubakia kwenye ligi hiyo.

"Timu yangu iko katika nafasi ya chini, nimedhamiria kuibadilisha na kuhakikisha tunafanya vizuri katika mechi zetu zijazo ili kujiweka katika mazingira mazuri ya kuendelea kucheza Ligi Kuu," alisema Odhiambo.

## Fainali Champion wa Kitaa zanukia

**Na Shufaa Lyimo**

MABONDIA wa ngumi za kulipwa, Salehe Mkalekwa na Maono Ally wamesaini mkataba wa kuzichapa katika fainali ya kumtafuta 'Champion wa Kitaa', zitakazofanyika Machi 20, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Mratibu wa pambano hilo, Bakari Hatibu alisema wanaendelea na mchakato wa kutafuta mahali ambapo pambano hilo litakapofanyika baada ya awali kutarajiwa kuchezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex.

"Hivi karibuni tutatangaza ni wapi fainali hizo zitafanyika na tayari tumeshasaini mikataba na Mkalekwa atazichapa dhidi ya Maono, likiwa ni pambano la kusindikiza fainali hizo za Champion wa Kitaa," alisema Bakari.

Aliongeza lengo la kuandaa mapambano hayo ni kuhakikisha wanakuza na kurejesha heshima ya mchezo wa ngumi nchini kwa kuwapa nafasi vijana wenye vipaji kuonyesha viwango vyao.

Aliwataja mabondia wengine watakaopigana kwenye fainali hizo ni pamoja na Abdallah Muhumba, Omary Salum, Peter Toshi, Swahibu Ramadhani, Said Uwezo, Mrisho Mzezele, Maneno Osward, Kennedy Samuel, Sebastian Deo na Hamadi Furahisha.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**UNITED KUSAJILI NYOTA**
MANCHESTER United ina uhakika wa kufikia malengo yao ya uhamisho msimu huu wa joto hata kama watashindwa kufuzu kwa Ligi ya Mabingwa Ulaya, huku kiungo wa kati wa West Ham ya England, Declan Rice mwenye umri wa miaka 23 na mshambuliaji wa Tottenham Hotspur (28), Harry Kane, akiwa kwenye orodha yao. ***(ESPN)***

**DEMBELE KUTUA PSG**
CHELSEA na Paris St-Germain wanaongoza katika kinyang'anyiro cha kumsajili mshambuliaji wa Ufaransa, Ousmane Dembele mwenye umri wa miaka 24 kwa uhamisho huru mara mkataba wake na Barcelona utakapokamilika msimu huu wa joto. ***(90min)***

**ISAK AGOMBEWA ULAYA**
KLABU ya Arsenal inakabiliwa na ushindani kutoka kwa Barcelona kumnunua mshambuliaji wa Real Sociedad, Alexander Isak mwenye umri wa miaka 22, ambaye ni mmoja wa walengwa wakuu wa kocha, Mikel Arteta. ***(Daily Express)***

**CESAR MAMBO SAFI**
BARCELONA wamempa mlinzi wa Hispania, Cesar Azpilicueta mkataba mpya wa miaka miwili ili kujiunga na klabu hiyo mara mkataba wa mchezaji huyo wa Chelsea mwenye umri wa miaka 32 utakapokamilika mwishoni mwa msimu huu. ***(Sport)***

**JOHNSON KIMEELEWEKA**
KLABU ya West Ham imechagua kumwongezea mkataba mlinzi wa pembeni wa England, Ben Johnson mwenye umri wa miaka 22 hadi mwaka 2024 ili kuzuia uwezekano wa kutakiwa na Arsenal, Tottenham na Liverpool.***(Mail)***

**SPURS WAMFUATA SIMON**
KLABU ya Tottenham Hotspur inavutiwa na mlinda mlango wa Athletic Bilbao na Timu ya Taifa ya Hispania, Unai Simon mwenye umri wa miaka 24, huku wakifikiria kuhusu mbadala wa muda mrefu wa Mfaransa, Hugo Lloris (35). ***(Marca)***

**BERARDI ANUKIA LEICESTER**
LEICESTER City wanaweza kufufua nia yao ya kumnunua winga wa Italia, Domenico Berardi ikiwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 ataamua kuondoka Sassuolo inayoshiriki Serie A msimu huu. ***(Leicester Mercury)***

**WEST YAMTAKA LONGSTAFF**
KLABU ya West Bromwich Albion wanamlenga kiungo wa kati wa England, Sean Longstaff mwenye umri wa miaka 24, ambaye alicheza chini ya kocha, Steve Bruce ndani ya Newcastle United. ***(Football League World)***

**MCCANN APATA ULAJI**
KOCHA wa zamani wa Hull City, Grant McCann mwenye miaka 41, amekubali dili la kuwa kocha wa Peterborough United. ***(Football Insider)***

**SPURS KUMUUZA BERGWIJN**
KLABU ya Tottenham ipo tayari kumuuza, Steven Bergwijn msimu huu wa joto huku AC Milan wakimtaka winga huyo wa Uholanzi mwenye umri wa miaka 24. ***(Calciomercato)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ARTETA, ARSENAL MAMBO YAMEIVA

Klabu hiyo yapanga kumpa mkataba mpya mnono ambao utamfanya awe kocha...

**LONDON, England**

KLABU ya Arsenal inajiandaa kumpa mkataba mpya kocha wake, Mikel Arteta na kumfanya kuwa miongoni mwa makocha watakaokuwa wanalipwa kiasi kikubwa cha fedha kwenye Ligi Kuu England.

Kwa mujibu wa gazeti la The Sun, Arsenal wako tayari kumpa mkataba mpya kwenye majira ya joto yanayofuata baada ya kuridhishwa na kazi aliyoifanya hadi sasa.

Mradi wake wa kukijenga kikosi cha washika bunduki hao wa London moja ya timu tishio zaidi unaonekana kwenda sawa.

Mkataba wake wa sasa na Arsenal unamalizika majira ya joto na ule mpya atakaopewa anatarajiwa kuvuna kiasi cha pauni milioni tano kwa mwaka, ni robo ya kiasi anacholipwa kocha wa Manchester City, Pep Guardiola.

Lakini Arteta alipoulizwa kuhusu kuelezea taarifa hizo hakuwa kwenye hali ya kutaka kujibu alinukuliwa akisema:

"Sikiliza, ni furaha kuwa hapa na kusudi langu ni kujenga klabu ambayo itakuwa na timu ya ushindi.

"Timu ambayo watu watafurahi kuingalia, timu ambayo wataitambua na kuibadilisha kutoka kwenye mpira tunaoutaka na kuwa kama taasisi."


LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 961,

MECHI KALI
SOUTHAMPTON
VERSUS
NORWICH CITY
1 | 1.56
X | 4.19
2 | 5.59

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# NEYMAR: NILIJARIBU KILA NJIA ILI KURUDI BARCELONA




**PARIS, Ufaransa**

MSHAMBULIAJI wa Paris Saint Germain, Neymar Junior amethibitisha alijaribu kufanya kila kitu awezacho ili kufanikisha uhamisho wake wa kurudi klabu yake ya zamani Barcelona kwenye dirisha la usajili majira ya joto mwaka 2019.

Mchezaji huyo wa kimataifa kutoka Brazil alihusishwa sana kurudi kwenye klabu yake hiyo ya zamani.

Neymar alisajiliwa na klabu ya PSG kwa uhamisho uliovunja rekodi ya dunia kwenye kipindi cha dirisha la usajili.

Mshambuliaji huyo mwenye miaka 30 alikuwa na shauku ya kutaka kuungana na mshambuliaji, Lionel Messi, ambaye kwa sasa amesajiliwa PSG baada ya Barcelona kukumbwa na matatizo ya kifedha na kuondoka akiwa mchezaji huru.

"Nilijaribu kurudi Barcelona, tulijaribu kila kitu, lakini haikuwezekana, nina furaha Lionel Messi amepata nafasi ya kuja PSG, yeye ni rafiki yangu na tunaishi vizuri," alisema Neymar akinukuliwa na jarida la France Football.

Neymar amethibitisha alifanya kadri awezavyo ili kurudi kwenye Ligi Kuu Hispania, LaLiga, ila kwa sasa anafuraha baada ya kuungana na mshindi huyo mara saba wa Ballon d'Or.

# Inter Milan kumuuza Martinez

**MILAN, Italia**

KLABU ya Inter Milan ipo tayari kumuuza mshambuliaji wake, Lautaro Martinez kwa euro milioni 90 msimu huu wa joto wakati Liverpool, Atletico Madrid na Borussia Dortmund ni miongoni mwa timu zinazomwania.

Kwa mujibu wa Sky Sport Italia, Martinez ndiye mchezaji anayewezekana kuwekwa kwenye soko la uhamisho mwishoni mwa msimu huu ili kusaidia kufadhili usajili wa wachezaji wapya.

Martinez alisajiliwa kwa euro milioni 25, Julai mwaka 2018 kutoka Racing na kuongeza mkataba wake Oktoba utakaodumu hadi Juni mwaka 2026.



Nyota huyo wa kimataifa wa Argentina amefunga mabao 12 katika mechi 33 za mashindano yote akiwa na Inter Milan msimu huu, lakini ameshindwa kufunga bao katika mechi saba zilizopita za Serie A.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, Martinez atauzwa kwa euro milioni 90, ikiwa imepunguzwa kwa kiasi kikubwa kutoka kwenye kifungu cha mkataba wake cha kumwachia kwa euro milioni 110.

Awali mchezaji huyo alikuwa akihusishwa na mpango wa kutakiwa Barcelona, lakini dili hilo likashindikana.

Na sasa Liverpool inaonekana ipo kwenye nafasi nzuri zaidi ya kumsajili ingawa inakabiliwa na ushindani kutoka Atletico Madrid na Borussia Dortmund.

HABARI MICHEZO

,840,460

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 26/02/22 | 18:00 | Brighton vs Aston Villa | 2.32 | 3.25 | 3.10 |
| 02. 26/02/22 | 18:00 | Brentford vs Newcastle | 2.41 | 3.25 | 2.95 |
| 03. 26/02/22 | 18:00 | Peterborough vs Hull City | 2.54 | 3.12 | 2.73 |
| 04. 26/02/22 | 18:00 | Millwall vs Sheffield Utd | 2.85 | 3.20 | 2.40 |
| 05. 26/02/22 | 18:00 | Birmingham vs Huddersfield | 2.50 | 3.24 | 2.70 |
| 06. 26/02/22 | 19:00 | Sivasspor vs Besiktas | 2.56 | 3.05 | 2.81 |
| 07. 26/02/22 | 20:30 | Oostende vs St Truiden | 2.47 | 3.40 | 2.66 |
| 08. 26/02/22 | 22:45 | Sassuolo vs Fiorentina | 2.75 | 3.44 | 2.47 |
| 09. 27/02/22 | 14:15 | AZ Alkmaar vs Feyenoord | 2.52 | 3.50 | 2.52 |
| 10. 27/02/22 | 15:30 | Hamburger SV vs Werder Bremen | 2.43 | 3.44 | 2.65 |
| 11. 27/02/22 | 16:00 | Alanyaspor vs Konyaspor | 2.45 | 3.16 | 2.86 |
| 12. 27/02/22 | 17:00 | Angers vs Lens | 2.80 | 3.25 | 2.50 |
| 13. 27/02/22 | 17:00 | Metz vs Nantes | 2.78 | 3.13 | 2.59 |

# MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## IJUMAA - 25/02/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 16:00 | 2093 | Geita Gold FC vs Namungo | 2.65 | 2.75 | 3.15 |
| 18:00 | 4710 | Radnicki Nis vs Novi Pazar | 1.80 | 3.37 | 4.04 |
| 18:00 | 4790 | Olympique Safi vs FUS Rabat | 2.84 | 3.03 | 2.39 |
| 18:30 | 2100 | UTA Arad vs Clinceni | 1.16 | 6.28 | 17.66 |
| 18:30 | 3614 | CSKA Sofia vs Botev Vratsa | 1.12 | 6.34 | 19.20 |
| 18:30 | 4878 | Coca Cola vs Arab Contractors | 2.36 | 2.91 | 3.26 |
| 19:00 | 2058 | Qrendi FC vs Fgura United | 3.07 | 3.65 | 2.00 |
| 19:30 | 3741 | NK Celje vs NK Aluminij | 1.63 | 3.71 | 4.62 |
| 20:00 | 1031 | Velez Mostar vs Zeljeznicar | 2.26 | 3.09 | 2.99 |
| 20:00 | 1817 | Omonia Nicosia vs Apoel Nicosia | 2.86 | 3.31 | 2.39 |
| 20:00 | 3112 | Adana Demirspor vs Antalyaspor | 1.86 | 3.51 | 3.96 |
| 20:00 | 4212 | Trabzonspor vs Kayserispor | 1.53 | 4.15 | 5.53 |
| 20:00 | 4246 | Denizlispor vs Boluspor | 3.48 | 3.43 | 1.92 |
| 20:00 | 4646 | Rakow Czestochowa vs Wisla Plock | 1.48 | 3.93 | 5.94 |
| 20:00 | 5063 | USM Alger vs NA Hussein Dey | 1.21 | 4.72 | 15.42 |
| 20:00 | 5482 | Pafos FC vs Aris Limassol | 2.13 | 3.12 | 3.57 |
| 20:00 | 5930 | Slaven Belupo vs Hrvatski Dragovoljac | 1.39 | 4.43 | 6.55 |
| 20:30 | 1862 | Fremad Amager vs Esbjerg | 2.81 | 3.29 | 2.27 |
| 20:30 | 3900 | Maritzburg Utd vs Golden Arrows | 2.13 | 2.93 | 3.71 |
| 20:30 | 4275 | Floridsdorfer AC vs Kapfenberg | 1.58 | 3.94 | 4.71 |
| 20:30 | 5015 | Hannover vs Holstein Kiel | 2.32 | 3.35 | 2.85 |
| 20:30 | 5817 | Paderborn vs Erzgebirge Aue | 1.50 | 4.32 | 5.49 |
| 20:45 | 3299 | AC Milan vs Udinese | 1.47 | 4.40 | 6.59 |
| 21:00 | 5265 | FC Helsingor vs Nykobing FC | 1.51 | 4.23 | 4.99 |
| 21:30 | 1360 | Universitatea Craiova vs Chindia Targoviste | 1.74 | 3.24 | 5.11 |
| 21:30 | 4614 | FC Stade LS Ouchy vs FC Vaduz | 2.10 | 3.47 | 2.98 |
| 21:30 | 4919 | Neuchatel Xamax vs SC Kriens | 1.50 | 4.15 | 5.22 |
| 21:30 | 5018 | FC Aarau vs FC Wil | 1.58 | 4.13 | 4.42 |
| 21:30 | 5556 | Yverdon-Sport FC vs FC Thun | 1.94 | 3.42 | 3.42 |
| 22:00 | 1340 | ADO Den Haag vs Telstar | 1.63 | 4.02 | 4.51 |
| 22:00 | 1351 | Paksi FC vs Videoton FC | 2.51 | 3.48 | 2.41 |
| 22:00 | 3237 | Almere City vs VVV Venlo | 1.98 | 3.42 | 3.47 |
| 22:00 | 5401 | Waalwick vs Twente | 3.05 | 3.29 | 2.23 |
| 22:15 | 1652 | FC Schaffhausen vs FC Winterthur | 2.15 | 3.47 | 2.89 |
| 22:25 | 3539 | FC Liefering vs Austria Lustenau | 2.01 | 3.67 | 3.04 |
| 22:30 | 2800 | Hoffenheim vs Stuttgart | 1.53 | 4.47 | 5.36 |
| 22:30 | 5855 | Legia Warszawa vs Wisla Krakow | 1.77 | 3.41 | 4.13 |
| 22:45 | 1113 | Treaty United vs Athlone Town | 1.71 | 3.56 | 4.24 |
| 22:45 | 1260 | Derry City vs Shamrock Rovers | 3.66 | 3.18 | 1.95 |
| 22:45 | 2209 | Hamilton vs Inverness | 2.88 | 3.22 | 2.34 |
| 22:45 | 4033 | Kfco Wilrijk vs Charleroi | 3.60 | 3.50 | 1.95 |
| 22:45 | 4217 | St Patricks vs Sligo Rovers | 1.90 | 3.18 | 3.86 |
| 22:45 | 5038 | Cork City vs Galway United | 2.31 | 3.18 | 2.84 |
| 22:45 | 5272 | Bohemians FC vs Dundalk FC | 2.30 | 3.14 | 2.89 |
| 23:00 | 1397 | Almeria vs Fuenlabrada | 1.52 | 3.82 | 6.27 |
| 23:00 | 2720 | Montpellier vs Rennes | 3.68 | 3.53 | 1.96 |
| 23:00 | 5812 | Southampton vs Norwich City | 1.56 | 4.19 | 5.59 |
| 23:00 | 5906 | Levante vs Elche | 2.00 | 3.40 | 3.75 |
| 23:00 | 5913 | Genoa vs Inter | 8.20 | 5.20 | 1.34 |
| 23:15 | 1627 | Belenenses vs Pacos Ferreira | 2.96 | 3.11 | 2.40 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# WAANDAAJI KILI MARATHON WAHIMIZA KUCHUKUA NAMBA

**Na Mwandishi Wetu**

WAANDAAJI wa mbio za Kilimanjaro Marathon wamewakumbusha washiriki kuzingatia muda uliotolewa wa kuchukua namba za kukimbia huku zoezi hilo likianza Moshi leo.

Hii imetokana na baadhi ya washiriki kufika katika vituo vya kutolea namba wakiwa wamechelewa na kutaka wahudumiwe wakati muda umeshakwisha.

"Tulishuhudia jambo hili wakati wa zoezi la Dar es Salaam pamoja na Arusha, na muda uliotolewa ulikuwa unatosha kabisa. Lakini baadhi ya washiriki walichelewa sana na hawakuweza kuhudumiwa kwa sababu tulikuwa tumefunga," ilisema taarifa ya waandaaji hao.

Kwa Moshi namba hizo zilianza kutolewa katika viwanja vya Chuo Kikuu Cha Ushirika jana na litamalizika kesho saa 11:00 jioni.

Waandaaji hao walisema mshiriki anaweza kumtuma mwakilishi amchukulie namba lakini lazima awe na nakala ya kitambulisho na ujumbe wa uthibitisho aliolipia kutoka Tigo.

Usajili kwa ajili ya mbio za kilomita tano bado unaendelea kwa kulipia fedha taslimu katika vituo vya kutolea namba.

Wadhamini wa mbio za Kilimanjaro Marathon 2022 ni Kilimanjaro Premium Lager (mdhamini mkuu) huku wadhamini wenza ni Tigo (kilomita 21) na Grand Malt (kilomita tano).

Wadhamini wa meza za maji ni pamoja na Absa Tanzania, Unilever Tanzania, TPC Sugar, Simba Cement na Kilimanjaro Water. Wasambazaji rasmi ni GardaWorld Security, Keys Hotel, Kibo Palace Hotel, CMC Automobiles na Surveyed Plots Company Ltd (SPC) na Bodi ya Utalii (TTB).

Mbio za Kilimanjaro Premium Lager Marathon mwaka huu zitafanyika keshokutwa katika viwanja vya Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), ambapo zimeandaliwa na taasisi ya Kilimanjaro Marathon Company Limited na kuratibiwa na wadau wa hapa nchini kampuni ya Executive Solutions Limited.

# Mhandisi Na Mkulima walamba Jackpot Bonus

**Na Mwandishi Wetu**

MHANDISI, Anganile Mbonile na Mkulima, Rafaeli Asenga wameshinda zaidi ya Sh. milioni 35 ya Jackpot Bonus ya SportPesa baada ya kupatia kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 za Jackpot ya wiki iliyoisha.

Wakizungumza katika ofisi za SportPesa jijini Dar es Salaam, baada ya ya hafla ya makabidhiano ya mfano wa hundi Rafaeli Asenga, mshindi wa Sh. milioni 26 ambaye ni Mkulima wa Kiteto, Manyara alisema alianza kucheza na Sportpesa tangu mwaka 2017 baada ya kushawishiwa na rafiki yake.

"Unajua pale ninapoishi kuna jamaa yangu Ismail Ramadhani Msuya alinipakulia App ya SportPesa na alinifundisha namna ya kucheza kwa kutumia simu yangu ya mkononi. Tokea hapo mimi ni kucheza na kushinda tu mara kwa mara.".

Naye anasema yeye alianza kucheza na Sportpesa kuanzia mwaka 2018 baada ya kusikia watu wanajishindia pesa kupitia mechi za kawaida na Jackpot kila wikiendi.

"Kama ilivyokuwa kwa watu wengi nina rafiki yangu Samuel Bundala ambaye yeye alinifundisha namna ya kucheza na kwa siku hiyo ilikuwa bahati yangu nilishinda zaidi ya elfu thelathini na hivyo kupata mwamko wa kucheza zaidi".

Wakizungumza namna walivyoweka mikeka yao Asenga anasema alitumia siku nne kufanya uchambuzi na utafiti kidogo kabla ya kuweka mkeka wa double combination siku ya Jumamosi mchana.

" Mimi nilitumia siku kama nne hivi mpaka kuweka mkeka huu nilioshinda. Baada ya hapo sikufuatilia kujua matokeo yamekwendaje. Ila nashukuru Mungu siku ya Jumapili mida ya saa nne kasoro usiku nilipata meseji ya ushindi huu wa Jackpot bonus ya milioni 26.




Mshindi wa Jackpot bonus, Rafaeli Asenga akishikilia mfano wa hundi ya Sh. milioni 26. 7 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 kwenye Jackpot ya SportPesa kupitia doble combination. Jackpot ya wiki hii ni Sh. milioni 961.8. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Michezo

Ijumaa Februari 25, 2022

Nipashe






## Arteta, Arsenal mambo yameiva



Kiungo wa Simba, Clatous Chama (katikati), akijaribu kumiliki mpira katika mazoezi ya timu hiyo kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya RS Berkane itakayochezwa keshokutwa nchini Morocco. **PICHA: SIMBA SC**

# YANGA YAFUNGUKA ILIPOISHIKA MTIBWA

●●●Yasema bao la Ntibazonkiza ndio liliwaongezea makali huku wapinzani wao...

**Na Adam Fungamwango**

IKIWA kileleni kwa tofauti ya pointi nane dhidi ya watani zao Simba, Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, amesema bao la kwanza walilolipata katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Mtibwa Sugar hapo juzi ndio liliifanya timu yao 'kuamka' na kupata ushindi katika mechi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Manungu Complex, Turiani mkoani Morogoro juzi.

Yanga ilipata ushindi wa mabao 2-0 na kufikisha pointi 39 wakati mabingwa watetezi, Simba yenye pointi 31 wako katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 16.

Akizungumza baada ya mechi hiyo, Kaze, raia wa Burundi alisema dakika 30 za kipindi cha kwanza zilimilikiwa na timu yake, lakini ilishindwa kuipenya ngome ya wapinzani kwa sababu wachezaji wake hawakuwa na kasi walipokuwa wakiingia kwenye eneo la hatari, hadi lilipopatikana bao hilo lililonekana kuwanyong'onyesha wenyeji.

"Hatukuanza mchezo vizuri, ndiyo maana tulicheza dakika 30 bila mashambulizi ya maana, tuliwamudu, lakini hatukuwa na spidi tulipokuwa tukiingia kwenye eneo la hatari. Na kwa kiasi kikubwa mechi iliamuliwa na bao la dakika za mwisho tulilolipata, hilo lilituridisha mchezoni na hata tulipoingia kipindi cha pili tulibadilika sana, tukaanza kucheza kama tulivyozoea, na tulikuwa na uwezo wa kufunga zaidi ya mabao mawili," alisema Kaze. Kuhusu ubingwa, Kaze alisema kazi bado inaendelea na hawawezi kujitamba tayari wamechukua ubingwa, badala yake wanachofanya ni kukusanya pointi tatu katika kila mechi ili baadaye huko mbele waangalie hali itakavyokuwa.

"Sisi tunachofanya ni kuilinda nafasi yetu ya kwanza kwa kukaa kileleni, na hii hailetwi na kitu chochote zaidi ya kupata pointi tatu kila mechi," alisema Kaze.

Baada ya kipigo hicho, Kocha Msaidizi wa Mtibwa Sugar, Awadh Juma, alisema kosa moja lililofanywa na beki wake kunyang'anywa mpira na Yanga kwenda kufunga bao ndilo lililowagharimu.

"Ukienda kucheza na timu ambayo ina wachezaji wazoefu matokeo yake ndiyo haya, tumefanya kosa moja tumeharibu mechi nzima. Tulianza vizuri, tulianza kwa kuwaheshimu na tulikuwa na uwezo wa kuwasimamisha, lakini tumewapa bao la kwanza wenyewe tu. Inauma kwa sababu tumepoteza nyumbani na tulikuwa na rekodi nzuri kwenye uwanja huu, lakini tunajipanga kwa mechi zinazofuata," alisema Awadh, kiungo wa zamani wa Mtibwa Sugar na Simba.

Kocha huyo aliongeza wataendelea kurekebisha makosa ili mechi za mzunguko wa pili ziwe na matokeo chanya ambayo yatawarejesha kwenye ushindani.

Alisema kihesabu bado hakuna uhakika wa timu yenye kutwaa ubingwa au zile ambazo zitachuka daraja, mechi bado ni nyingi na lolote linaweza kutokea.

"Tutapambana, tumekuwa na mzunguko wa kwanza wenye changamoto, sasa tunaingia kwenye mzunguko wa mwisho, huku ndio hesabu kamili zinapigwa, hatutakiwi kurudia kile tulichofanya mwanzoni mwa msimu," Awadh aliongeza.

Mtibwa Sugar itaanza hesabu zake za mzunguko wa pili ugenini jijini Mbeya kesho kwa kuwakabili Mbeya Kwanza kwenye Uwanja wa Sokoine.

## Simba yaendeleza ukachero Morocco

**Na Saada Akida**

KATIKA kuhakikisha inapata matokeo mazuri hapo kesho, benchi la ufundi la Simba linaloongozwa na Kocha Pablo Franco amefanikiwa kuwasoma wapinzani wao, RS Berkane kwa kuwatizama kwenye mechi yao ya Ligi Kuu ya Morocco dhidi ya vigogo wenzao, FAR Rabbat.

RS Berkane watakuwa nyumbani kuwakaribisha Wekundu wa Msimbazi katika mechi ya Kundi D ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Municipal de Berkane.

Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola, aliliambia gazeti hili jana usiku walitarajia kupata nafasi nyingine ya kuona ubora na udhaifu wa wapinzani wao wakicheza mechi ya ligi.

Matola alisema licha ya kuendelea kuandaa kikosi chao, kupitia video za mechi zilizopita za RS Berkane lakini ana imani mchezo wao jana utawapa nafasi ya kufahamu zaidi na kuimarisha mikakati ya kuwadhiti pale watakapokutana nao Jumapili.

Kocha huyo alisema baada ya kufika jijini Casablanca, kikosi cha timu hiyo kitafanya mazoezi ya utimamu wa mwili kwa sababu tangu walipomaliza mchezo dhidi ya US Gendarmerie hakijapata muda wa kupumzika vizuri.

Aliongeza wamejiandaa kukutana na ushindani mkubwa kwa sababu wapinzani wao watakuwa nyumbani lakini walipoteza mchezo uliopita dhidi ya Asec Mimosas ugenini Ivory Coast.

"Tunaandaa timu yetu kupata matokeo mazuri kuelekea mchezo huo, tumefanyia kazi mapungufu yetu kuhakikisha tunarejea na pointi muhimu katika mchezo wetu dhidi ya RS Berkane, mechi zote kwenye hatua hii ni ngumu, hata kucheza ugenini," alisema Matola.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez, alisema kikosi cha timu hiyo kitaondoka Casablanca leo kuelekea Berkane tayari kwa mchezo wa keshokutwa.

"Kikubwa mashabiki wa Simba watuombee dua tuweze kufanya vizuri, timu yetu iko vizuri na wachezaji wanaenda kupambana kuhakikisha tunarejea na pointi nyingine nyumbani badala ya tulizopata katika mchezo uliopita dhidi ya USGN Gendarmarie," alisema Barbara.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >